**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO**

# MWELEKEO WA MPANGO WA TAIFA NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2024/2025

**FEBRUARI, 2024**

**INAWASILISHWA KWA:**

**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**YALIYOMO**


1. UTANGULIZI ....................................................................................3
2. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2022/2023 (JULAI-JUNI) .................................................................................7
3. TAARIFA YA MWENENDO WA HALI YA UCHUMI KWA KIPINDI CHA JULAI-DISEMBA 2023 ....................................................................10
4. UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO ....................................21
5. UTEKELEZAJI WA BAJETI JULAI-DISEMBA 2023/2024......................37
6. MISAMAHA YA KODI KWA KIPINDI CHA JULAI –DISEMBA 2023 .........52
7. UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA SERA ZA MAPATO KWA KIPINDI CHA JULAI DISEMBA 2023 ..................................................................53
8. MABADILIKO YA MAFUNGU YA BAJETI KWA KIPINDI CHA JULAI – DISEMBA MWAKA 2023/2024 ..............................................................55
9. MPANGO WA SERIKALI WA UNUNUZI WA MAGARI .............................56
10. MPANGO WA SERIKALI WA MATUMIZI YA ARDHI ..........................58
11. MATARAJIO (LIKELY OUTTURN) YA MAPATO NA MATUMIZI JULAI-JUNI KWA MWAKA 2023/2024 ..........................................................59
12. MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2024 ....................63
12.1. Uchumi wa Dunia ........................................................................63
12.2. Mwelekeo wa hali ya uchumi wa Zanzibar 2024 ............................63
12.3. Misingi ya Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2024/25................64
12.4. Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi...................................65
12.5. Mwelekeo wa Mfumko wa Bei Zanzibar .........................................65
13. MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2024/2025 MAPENDEKEZO YA MAENEO YA KIMKAKATI ................66
13.1. MAENEO YA KIMKAKATI KWA MWAKA 2024/25 ...........................67
**14. MAPENDEKEZO YA SURA YA BAJETI MWAKA WA FEDHA 2024/2025** ..........................................................................70
**13.1 Mwelekeo wa Ukusanyaji wa Mapato** .......................................71
**13.2 Mapendekezo ya Mgao wa Matumizi** .......................................72
15. MIKAKATI YA UPATIKANAJI WA RASILIMALI FEDHA........................72
16. MALENGO MAKUU YA SERIKALI .....................................................73
17. UGHARAMIAJI WA NAKISI YA BAJETI. ............................................73
18. VIPAUMBELE VYA KIBAJETI (VIGEZO VYA UGAWAJI WA RASILIMALI) KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ................................................73
**19. HITIMISHO** .....................................................................74
20. VIAMBATISHO.............................................................................75

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia neema ya uhai na afya na kutubarikia amani inayoendelea kutawala ndani nchi yetu, ambapo kwa pamoja vimetuwezesha kuwa hapa leo nami kupata fursa ya kusimama mbele ya Baraza hili ili kuwasilisha Mwelekeo wa Mpango wa Taifa na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Mwelekeo huu una wasilishwa kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 106 cha Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 (kama ilivyorekebishwa) ambacho kinaitaka Wizara inayosimamia masuala ya fedha, kabla ya kumalizika mwaka wa fedha, kutayarisha na kuwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka unaofuata kwa ajili ya kuidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika,** Moja ya jukumu la msingi la Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango kwa mujibu wa **Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya Mwaka 2016, kifungu cha 41(1)** ni kuandaa Mipango wa Maendeleo na kufanya makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali. Kifungu hicho kinamtaka Waziri anayehusika na masuala ya fedha, kutayarisha Mpango wa Maendeleo na Mwelekeo wa Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka unaofuata na kuuwasilisha katika mamlaka zinazohusika kwa kuidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika,** Maagizo hayo ya kisheria yanakwenda sambamba na lengo la kukidhi **Kanuni ya Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka 2020 kifungu 93 (1) – (4)** ambavyo vinaitaka Serikali kuwasilisha **Mwelekeo wa Mpango wa Taifa** katika mkutano wa Baraza la Wawakilishi kwa jili ya kupokea mawazo, michango na ushauri na hatimae kupata ridhaa ya Wajumbe wa Baraza.

**Mheshimiwa Spika,** Mwelekeo wa Bajeti hutumika kama dira kwa Serikali kuweza kuonesha sera na mikakati pamoja na mahitaji ya rasilimali fedha zinazohitajika katika utekelezaji wa vipumbele vya Taifa na kufanikisha malengo iliyojipangia kwa mujibu wa rasilimali zilizopo na zinazotarajiwa kupatikana.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali inaendelea na mkakati wa kuibadilisha taswira ya Zanzibar (maendeleo ya kiuchumi na kijamii) kupitia utekelezaji wa miradi ya kimkakati katika maeneo ya uzalishaji, kugharamia utoaji wa huduma muhimu za kijamii ikiwemo afya, elimu, maji, umeme, kuimarisha utalii na uwekezaji kwa lengo la kuinua kipato cha mwananchi na uchumi wa Zanzibar kwa ujumla wake.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi wa huo juu ya matakwa ya kisheria, napenda kuchukua fursa hii, kwa heshima kubwa na namna ya pekee, kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi** kwa kuendelea kuniamini katika dhamana hii kubwa na nzito ya kusimamia na kuongoza Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango. Kwa dhati ya moyoni naomba nikiri kuwa

miongozo na maelekezo yake yamekuwa yakinitia moyo wa kupambana na kufanya kazi bila ya kuchoka.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba pia kuwapongeza wasaidizi wakuu wa Mheshimiwa Rais, ambao ni **Makamo wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Othman Masoud Othman** na **Makamo wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah.** Hakika uongozi wao, busara zao na kujitoa kwao kumetujenga sisi Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza majukumu yetu kwa mashirikiano na kuvumiliana katika kiwango cha juu kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kuchukua nafasi hii, kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wote walioteuliwa akiwemo; **Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Mheshimiwa Shaaban Ali Othman, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mheshimiwa Shariff Ali Shariff, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Ikulu Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir na Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mheshimiwa Mudrik Ramadhan Soraga**. Kipekee nimpongeze, **Naibu Waziri - Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Mheshimiwa Juma Makungu Juma,** alikotoka alifanikiwa sana kusaidia kutatua migogoro ya ardhi, kwa kuwa sasa ameingia katika masuala ya fedha, matumaini yangu, uzoefu wake utasaidia pia kutatua changamoto za kisera na kiutendaji zinazohusu fedha na mipango. Kwa niaba ya viongozi na watendaji wote wa Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango na Taasisi zake zote, tunamuahidi kumpa mashirikiano ili tusaidiane katika kusogeza mbele maendeleo yaliyo kwishakupatikana ndani ya Taifa hili.

**Mheshimiwa Spika,** Bila kusahau pongezi zangu za kipekee kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakiongozwa na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi **Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid** na Wasaidizi wako wote wakiwemo Mheshimiwa **Naibu Spika** pamoja na Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu pamoja na Wajumbe wote Baraza hili. Hakika ushauri wenu na miongozo yenu imetuwezesha kwa kiasi kikubwa, kutimiza takwa hili la kikatiba leo hii.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba pia, nitoe pole kwa familia na Watanzania wote kufuatia Msiba wa aliyekuwa **Waziri Mkuu Mstaafu Edward Ngoyai Lowassa.** Kwa hakika kifo chake kimetugusa sana, sisi kama sehemu ya viongozi wa Taifa hili, tulitamani sana kuwa nae kuendelea kuchota hazina ya mawazo, fikra na falsafa ya uongozi na misingi yake, lakini mwisho wa siku tunamalizia na kauli isemayo **Hakika Sisi Sote ni wa Allah na Kwake Tutarejea.** Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema anapostahiki.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa kwa ruhusa yako, naomba kutoa hoja kuwa Baraza lako tukufu, lipokee na kujadili **Mwelekeo wa Mpango wa Taifa na Bajeti ya Serikali Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.** Mwelekeo huu, unawasilishwa pamoja na muhutasari wa taarifa zifuatazo:

i. Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/2023 (Julai-Juni)

ii. Mwenendo wa Hali ya Uchumi kwa Kipindi cha Julai-Disemba 2023.
iii. Hali ya Deni la Taifa la Zanzibar;
iv. Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali ya mwaka 2023/24 kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2023;
v. Matarajio ya ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali hadi kumalizika kwa mwaka wa fedha 2023/2024;
vi. Mwelekeo wa Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2024;
vii. Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2024/2025; na
viii. Mapendekezo ya Sura ya Bajeti kwa Mwaka 2024/2025.

## 2. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2022/2023 (JULAI-JUNI)

### 2.1. Mapato

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali ilipanga kukusanya **TZS 2,606.58 bilioni. Kati ya fedha hizo, Serikali ni TZS 2,572.70 bilioni na Mamlaka za Serikali za Mitaa ni TZS 33.88 bilioni.** Kati ya fedha zilizopaswa kukusanywa kwa upande wa Serikali ni TZS 1,234.2 bilioni zinatokana na mapato ya ndani na TZS 1,388.6 bilioni zinatokana na mapato mengineyo. Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yalipangwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani TZS 17.6 bilioni na TZS 16.28 bilioni ni bajeti ya ziada ya mkopo kutoka Benki ya CRDB kwa mamlaka za Serikali za Mitaa zilizotumika katika ujenzi wa Masoko.

## 2.2. Utekelezaji Halisi

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi kilichoishia Juni Mwaka wa Fedha 2022/2023, **mapato ya Serikali yalifikia TZS 1,590.3** bilioni sawa na asilimia 61.8 ya makisio ya ukusanyaji wa TZS 2,572.70 bilioni. Makusanyo haya yanajumuisha mapato ya ndani ya TZS **1,193.1** bilioni na mapato mengineyo ya TZS **397.3** bilioni. Kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, makusanyo yalifikia TZS **30.58** bilioni sawa na asilimia 90.47 ya kukusanya 33.88 bilioni.

### 2.2.1. Mapato ya Ndani

**Mheshimiwa Spika,** Mapato ya ndani yamejumuisha:

i. Mapato yatokanayo na kodi TZS 1,038.3 bilioni sawa na asilimia 98.5 bilioni ya makadirio ya TZS 1,054.9 bilioni (ZRA TZS 565.9 bilioni, TRA TZS 451.4 bilioni na PAYE transfer TZS 21 bilioni) na

ii. Mapato yasiyokuwa ya kodi ni TZS 154.8 bilioni sawa na asilimia 86.2 ya makadirio ya TZS 179.5 bilioni.

### 2.2.2. Mapato Mengineyo

**Mheshimiwa Spika,** Mapato mengineyo yamejumuisha:

i. Fedha zilizopatikana kutokana na mikopo na misaada ni TZS 172.4 bilioni

ii. Marejesho ya Mkopo wa Exim Benki ya China yalifikia TZS 130.4 bilioni

iii. TZS 27.1 bilioni zilipatikana kutokana na Serikali kukopa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

iv. Misaada ya Kibajeti (GBS) TZS 67.4 bilioni

### 2.3. Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Serikali ilikadiria kutumia jumla ya **TZS 2,572.70 bilioni,** ikihusisha matumizi ya kazi za kawaida ya **TZS 1,220.5 bilioni** na kazi za maendeleo **TZS 1,352.2** bilioni.

**Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa, zilikadiria kutumia TZS 33.88 bilioni.**

### 2.4. Utekelezaji Halisi

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai-Juni Mwaka wa Fedha 2022/2023, matumizi halisi yalifikia TZS 1,453.7 bilioni sawa na asilimia 66 ya Makadirio ya TZS 2,572.7 bilioni. Matumizi hayo yanajumuisha:

#### 2.4.1. Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya kawaida TZS 993.0 bilioni zimetumika sawa na asilimia 94.6 ya makadirio ya TZS 1,220.5 bilioni. Uchambuzi ufuatao unahusika na matumizi hayo.

i. **Mishahara** ni TZS 626.8 bilioni sawa na asilimia 99.6 ya makadirio ya kutumia TZS 628.7 bilioni;

ii. **Matumizi mengineyo** yamefikia TZS 194.4 bilioni sawa na asilimia 50.9 ya makadirio ya TZS 381.6 bilioni;

iii. Matumizi ya **Mfuko Mkuu wa Serikali** yamefikia TZS 171.7 bilioni sawa na asilimia 81.7 ya makadirio ya TZS 210.3 bilioni.

**Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa** yamefikia TZS 30.58 sawa na asilimia 90.26 ya makadirio ya kutumia TZS 33.88 bilioni.

### 2.4.2. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi ya miradi ya maendeleo ya Serikali, yalifikia TZS 460.7 bilioni sawa na asilimia 34.1 ya makadirio ya kutumia 1,352.2 bilioni.

Kiasi cha TZS 308.9 bilioni zimetokana na fedha za mapato ya ndani ambapo ni sawa na asilimia 45.3 ya makadirio ya TZS 682.5 bilioni na TZS bilioni 151.8 bilioni zimetokana na Washirika wa Maendeleo ikihusisha Misaada na Mikopo sawa na asilimia 22.7 ya makadirio ya TZS 669.7 bilioni (**Kiambatisho namba 1 kinahusika.**

## 3. TAARIFA YA MWENENDO WA HALI YA UCHUMI KWA KIPINDI CHA JULAI-DISEMBA 2023

**Mheshimiwa Spika,** Hali ya uchumi ndio msingi wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya nchi yoyote. Mipango hiyo inategemea viashiria vya uchumi jumla vikiwemo mfumko wa bei, sekta ya nje, upatikanaji wa ajira na uwekezaji. Mwenendo wa hali ya uchumi wa dunia una athari ya moja kwa moja na uchumi wa Zanzibar. Hii ni kutokana na mwingiliano wa kibiashara na uhusiano wa kimataifa pamoja na shughuli za kiuchumi zinazochangia ukuaji wa Pato la Taifa ikiwemo utalii. Taarifa hii, inaonesha hali ya uchumi wa dunia, Afrika Mashariki na Zanzibar pamoja na hali ya mfumko wa bei katika maeneo hayo.

### 3.1. Ukuaji wa Uchumi wa Dunia

**Mheshimiwa Spika,** Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi wa Dunia (World Economic Outlook, Februari 2024) ya

Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) inaonesha kuwa katika kipindi cha Julai – Disemba 2023, uchumi wa dunia umeimarika na kukua kwa wastani wa asilimia 2.7 ukilinganisha na ukuaji wa wastani wa asilimia 1.9 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji huo unatokana na kuimarika kwa masoko ya fedha kwa nchi za Marekani na China ambazo zimeongeza uwekezaji katika nchi zao na hivyo kuongeza ajira na shughuli za kiuchumi.

### 3.2. Uchumi wa Nchi za Afrika Mashariki

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha tathmini, kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi za Afrika Mashariki umekuwa na kufikia wastani wa asilimia 5.1 kutoka asilimia 4.4 iliyorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Hii inatokana na kuimarika kwa uwekezaji kwa nchi hizo pamoja na kuongezeka kwa thamani kwa baadhi ya madini na kuimarika kwa miundombinu.

### 3.3. Mfumko wa Bei Duniani

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha miezi sita (Julai-Disemba 2023) kasi ya mfumko wa bei duniani imepungua kufikia wastani wa asilimia 6.9 kutoka asilimia 8.6 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022. Kupungua kwa mfumko wa bei kumetokana na kupungua kwa bei za bidhaa za chakula duniani kama vile mchele, ngano, sukari, mafuta ya kupikia na bidhaa zisizo za chakula zikiwemo nishati ya mafuta, mbolea, gesi na bidhaa za chuma.

### 3.4. Mfumko wa Bei kwa Nchi za Afrika Mashariki

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miezi sita (Julai-Disemba 2023) kasi ya mfumko wa bei kwa nchi za Afrika Mashariki imefikia wastani wa asilimia 11.1

kutoka wastani wa asilimia 14.5 kipindi kama hicho mwaka 2022. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji pamoja na kupungua kwa gharama za uagiziaji wa bidhaa za chakula na zisizo za chakula katika kipindi hicho ikiwemo nishati ya mafuta kutoka nje ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

### 3.5. Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha tathmini kasi ya ukuaji wa uchumi imefikia wastani wa asilimia 7.6 kutoka wastani wa asilimia 6.3. Ukuaji wa uchumi wa Zanzibar umetokana na kuongezeka kwa idadi ya watalii kufikia 356,459 kutoka watalii 345,300 waliorikodiwa kuingia katika kipindi kama hicho mwaka 2022 ikiwa ni ongezeko la asilimia 3.2. Vile vile, ukuaji huu umetokana na kuimarika kwa shughuli za uvuvi kufikia ukuaji wa asilimia 2.9 (kutoka 2.6), ujenzi asilimia 0.1 (kutoka -0.5), biashara za jumla na reja reja kufikia wastani wa asilimia 0.8 (kutoka 0.7) na sekta ndogo ya mazao kufikia wastani wa asilimia 1.0 (kutoka 0.8). Ukuaji huo umekwenda sambamba na kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato. Mchango wa Sekta katika ukuaji wa uchumi ni kama ifuatavyo:

#### i. Sekta ya Huduma

**Mheshimiwa Spika, Sekta ya Huduma** inajumuisha huduma za chakula na malazi, elimu, afya, huduma za kifedha, bima na mawasiliano. Sekta ya huduma imeendelea kuwa ndio sekta inayoongoza katika kuchangia uchumi wa Zanzibar Kwa kipindi cha Julai – Disemba 2023, mchango wa sekta hii umefikia asilimia 53.9 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 55.9 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022.

ii. **Sekta ya Viwanda**

**Mheshimiwa Spika, Sekta ya Viwanda** ambayo inajumuisha sekta ndogo za uchimbaji mawe na mchanga, viwanda vidogo vidogo, umeme, maji na ujenzi. Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2023 **sekta ya viwanda imechangia wastani wa asilimia 20.7** kutoka wastani wa asilimia 19.9 iliyorikodiwa kwa kipindi kama hicho mwaka 2022.

iii. **Sekta ya Kilimo**

**Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo,** inajumuisha sekta ndogo ya mazao, uvuvi, misitu na ufugaji. Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2023; **sekta ya kilimo imechangia wastani wa asilimia 26.2** kutoka wastani wa asilimia 24.1 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022.

### 3.6. Hali ya Mfumko wa Bei Zanzibar

**Mheshimiwa Spika,** Kasi ya mfumko wa bei imefikia **wastani wa asilimia 6.5 katika kipindi cha miezi sita** (Julai hadi Disemba mwaka 2023) ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.6 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022. Kupungua kwa mfumko wa bei, umetokana na **kupungua kwa baadhi ya bidhaa zisizo za chakula kufikia asilimia 3.1 kutoka asilimia 4.8.** Kupungua huku kumechangiwa na kupungua kwa bei za baadhi ya huduma zikiwemo, usafiri wa ndani, bidhaa za nguo, baadhi ya bidhaa za huduma za mahoteli, vifaa vya umeme wa jua na nyingi nyenginezo. Hata hivyo, mfumko wa bei kwa bidhaa za chakula umepanda kutoka wastani wa asilimia 9.3 (Julai – Disemba, 2022) hadi asilimia 11.5 (Julai – Disemba 2023). **Mfumko wa bei kwa bidhaa za chakula ulifikia wastani wa asilimia 11.5 kwa**

**kipindi cha tathmini kutoka wastani wa asilimia 9.3** kwa kipindi kama hicho mwaka 2022 na bidhaa zisizo za chakula kufikia wastani wa asilimia 3.1 kutoka wastani wa asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, **bei za baadhi ya bidhaa za chakula hususan zile zinazopatikana ndani** zimepungua kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji na kuimarika kwa miundombinu ya usafiri wa ndani. Bidhaa hizo ni kama vile samaki kutoka TZS 9,903 kwa kilo hadi kufikia TZS 9,091 kwa kilo, ndizi mbichi kutoka TZS 1,375 kwa kilo hadi kufikia TZS 1,212 kwa kilo, muhogo kutoka TZS 909 kwa kilo hadi TZS 658, kwa kilo, kuku wa kienyeji kutoka TZS 15,250 hadi TZS 12,723 na mbatata kutoka TZS 1,686 kwa kilo hadi TZS 1,300 kwa kilo.

**Mchoro nambari 1: Mfumko wa bei wa Zanzibar kwa kipindi cha miezi sita (Julai – Disemba)**




**Chanzo, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, 2023.**

### 3.7. Uingiaji wa Watalii

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai – Disemba 2023, idadi ya watalii imeongezeka na kufikia watalii

356,459 ikilinganishwa na watalii 345,300 ambao **wameingiza takriban TZS 67.30** bilioni kutoka TZS 59.90 bilioni kwa kipindi kama hicho mwaka 2022. Ongezeko hilo limesababishwa na jitihada kubwa zinazochukuliwa na Serikali za kuitangaza Zanzibar kimataifa, kuendelea kuimarika kwa hali ya amani na utulivu nchini, kuongezeka kwa mawakala wa usafirishaji watalii pamoja na kuitangaza Zanzibar kiutalii kupitia maonyesho ya nje na ndani ya nchi. Jitihada nyengine ni kushiriki katika makongamano ya kibiashara na uwekezaji katika mataifa mbali mbali duniani; Mabalozi wa Tanzania walioko nje ya nchi kuendelea kuutangaza utalii wetu; pamoja na kufunguliwa kwa miradi mikubwa pamoja na hoteli za nyota tano.

**Mchoro Nam 2. Mwenendo wa Uingiaji wa Watalii Julai-Decemba 2022/2023**




**Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, 2023.**

### 3.8. Uagiziaji na Usafirishaji wa Biashara Nje ya Nchi

**Mheshimiwa Spika,** Kuwepo kwa uagiziaji zaidi wa bidhaa kuliko usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi

kumepelekea kuongezeka kwa nakisi ya biashara. Katika kipindi cha Julai-Disemba 2023, nakisi ya biashara imeongezeka na kufikia **thamani ya TZS 744.5 bilioni** ikilinganishwa na TZS 558.8 bilioni kwa kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 33.2.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha tathmini, thamani ya usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi imepungua na kufikia **TZS 73.8 bilioni** kutoka thamani ya **TZS 113.8 bilioni** kwa kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 35.1. Usafirishaji wa zao la karafuu kwa kipindi cha Julai-Disemba 2023, umepunguwa kufikia tani 1,405 zenye thamani ya **USD 11.9 milioni** kutoka tani 3,850 zenye thamani ya **USD 31.4 milioni** kwa kipindi kama hicho mwaka 2022. Hii imesababishwa na msimu mdogo wa zao hilo pamoja na kupungua kwa usafirishaji wa bidhaa za chakula kufikia thamani ya **TZS 55.6 bilioni** kutoka thamani ya **TZS 103.5 bilioni** kwa kipindi kama hicho mwaka 2022.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuchukuwa hatua za kuimarisha zao la karafuu ili kuongeza mapato na kuchangia uchumi wa nchi kwa kiasi kikubwa. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na kuanza na matayarisho ya utafiti mkubwa wa zao hilo kuanzia uzalishaji, usafirishaji na uuzaji pamoja na kuangalia namna bora ya usimamizi na uendeshaji wa zao hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelekea kuchukua jitihada mbalimbali za kimkakati ili kukuza uchumi kwa kuongeza uzalishaji na usarifu wa bidhaa za

ndani ili kuongeza thamani ya usafirishaji wa bidhaa zetu nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Ukuaji wa uchumi wa Zanzibar wa asilimia 7.1 inaleta sura katika kuboresha hali za wanachi kwa kuimarika na kuongezeka kwa huduma za kijamii katika maeneo mengi zikiwemo;

i. Kuongezeka kwa vituo vya afya ambavyo vimepelekea kupatikana kwa huduma za afya kwa urahisi na kwa karibu. Baadhi ya matokeo ni pamoja na kupungua kwa vifo vya watoto wachanga kutoka 2035 hadi 1,727 mwaka 2023.

ii. Kuongezeka kwa ujenzi wa skuli na kupelekea kupunguza mrundikano wa wanafunzi kwenye madarasa na kupunguza masafa ya upatikanaji wa elimu. Kwa mwaka uliopita, madarasa 1,131 yalijengwa na wastani wa wanafunzi kwa darasa moja la wanafunzi imefikia 45 kutoka wastani wa wanafunzi 80 mwaka 2021

iii. Kuimarika kwa miundombiu ya barabara ambayo inasaidia kurahisisha usafirishaji wa abiria, mizigo na shughuli za kiuchumi. Katika kipindi cha mwaka mmoja, kilomita zipatazo 82.8 zimejengwa.

iv. Ujenzi wa masoko ambao utasaidia kuongeza hamasa ya uzalishaji wa ndani kwa vijana na kupelekea upatikanaji wa ajira. Masoko mbali mbali yanaendelea kujengwa katika maeneo ya Unguja na kwa Pemba.

v. Upatikanaji wa maji safi na salama umefikia wastani wa asilimia 70 kutoka asilimia 55 asilimia mwaka 2022. Baadhi ya miradi iliyokamilika ni pamoja na Mradi unafadhiliwa na Benki ya Exim ya India (ambayo imekamilisha Schemes za Dimani, Masingini na Dole) na Schemes za Chanjaani, Kendwa na Makangale.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai-Disemba 2023, thamani ya uagiziaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi imeongezeka na kufikia **TZS 818.4 bilioni** ikilinganishwa na **TZS 672.7 bilioni** kwa kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 21.6. Kuongezeka kwa thamani ya uagiziaji kumetokana na kuongezeka kwa uagiziaji wa bidhaa ya nishati ya mafuta kufikia **TZS 368.3 bilioni** kutoka **TZS 304.2 bilioni** kwa kipindi kama hicho mwaka 2022.

### 3.9. Upatikanaji wa ajira

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai – Disemba mwaka 2023, ajira mpya zilizopatikana **ni 11,395** ukilinganisha na ajira mpya **9,426** zilizopatikana katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Kati ya ajira hizo mpya, ajira 932 ni kutoka Serikalini, ajira kutoka sekta binafsi ni 6,448 na ajira za nje zimefikia 1,553. Ajira zilizopatikana kutokana na miradi ya uwekezaji zimefikia **2,462** ukilinganisha na **ajira 3,650** katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

**Mheshimiwa Spika,** Hali ya ukosefu wa ajira kwa Zanzibar inaendelea kupunguwa kutokana na jitihada mbali zinazochukuliwa na Serikali kwa sasa ikiwemo uwekezaji, ujenzi wa miundo mbinu ya bandari barabara na maeneo mengine, kwa sasa kutokana na

ripoti ya matokeo ya mwaka 2022 hali ya ukosefu wa ajira inakadiriwa kufikia asilimia 9.9 kutoka asilimia 14.1 kwa mwaka 2014.

**3.10. Miradi ya Uwekezaji.**

**Mheshimiwa Spika,** Idadi ya miradi iliyowekezwa nchini katika kipindi cha Julai – Disemba mwaka 2023 imefikia miradi 57 yenye thamani ya **USD 1.46 bilioni** kutoka miradi 42 yenye thamani ya **USD 245 milioni.** Serikali inaendelea na jitihada za kuitangaza Zanzibar kiuwekezaji sambamba na kuendelea kuwawekea mazingira mazuri wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuja kuwekeza kwa maendeleo endelevu ya Zanzibar.

**3.11. Mwenendo wa Thamani ya Sarafu ya Tanzania**

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai-Disemba 2023 sarafu ya Tanzania ilibadilishwa kwa wastani wa **TZS 2,454.10** kwa Dola ya Kimarekani ikilinganishwa na wastani wa **TZS 2,306.84** katika kipindi kama hicho cha mwaka 2022. Hii ni kutokana na kuendelea kupanda kwa uhitaji wa dola na kupunguwa kwa mzunguko wa fedha za kigeni ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Hali ya upatikanaji wa fedha za kigeni nchini imeendelea kuwa himilivu wa wastani. Hii inatokana na kuendelea kuwepo kwa akiba ya fedha za kigeni, ambapo hadi kufikia mwezi Disemba 2023, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa **Dola za Marekani bilioni 5.5,** ambayo inatosheleza miezi 4.5 ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kudhibiti sarafu ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani, Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kuchukua hatua zifuatazo:-

i. Kununua dhahabu kutoka kwa wachimbaji kwa ajili ya kuweka dhamana katika masoko ya fedha ya nje ili kuweza kupata Dola za Marekani.
ii. Kuendelea kushirikisha benki za biashara, maduka ya kubadilisha fedha za kigeni, pamoja na wadau wengine katika kusimamia Sheria, Kanuni na Miongozo ya fedha za kigeni nchini.
iii. Kutekeleza Sera ya Fedha kwa kutumia Viwango vya Riba ili kuweza kuimarisha uchumi wa nchi na kudhibiti uwezekano wa sarafu ya Tanzania kupungua thamani zaidi.
iv. Kusimamia muongozo wa shughuli za kununua au kuuza fedha za kigeni nchini kufanyika na taasisi za fedha zilizoidhinishwa na Benki Kuu ya Tanzania pekee. Hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Kigeni 1992 (4). Lengo ni kukabiliana na biashara haramu ya fedha za kigeni, ikiwemo soko lisilo rasmi (black market or parallel foreign exchange market).
v. Kusisitiza matumizi ya bidhaa na huduma zinazozalishwa ndani ya nchi. Hatua hii itapunguza mahitaji ya fedha za kigeni, kuimarisha shughuli za uchumi, na kuongeza kipato kwa wananchi. Hatua hii itapunguza uhitaji wa kuagiza bidhaa au huduma kutoka nje.

**Mheshimiwa Spika,** Hatua hizi, zimewezesha kupunguza kasi ya kupungua kwa thamani ya shilingi ya Tanzania. Hata hivyo, ili kuwezesha thamani ya sarafu ya Tanzania kuimarika, Serikali inaendelea

kuweka sera madhubuti za uzalishaji wa ndani ili na kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa kutoka nje.

### 3.12. Mwenendo ya Deni la Taifa

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Disemba 2023 Deni la Zanzibar limefikia TZS 884.7 bilioni kutoka TZS 331.93 bilioni katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Kati ya deni hilo, deni la ndani ni TZS 870.3 bilioni sawa na asilimia 98 na deni la nje linalodhaminiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni TZS 14.4 bilioni sawa na asilimia 2. Kwa deni la hadi **mwezi Disemba 2022,** deni la ndani lilikuwa TZS 318.69 bilioni sawa na asilimia 96 ya deni lote na deni la nje lilikuwa TZS 13.24 bilioni sawa na asilimia 4 ya deni lote.

Deni linalodhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upande wa Zanzibar hadi kufikia Disemba 2023, ni TZS 2,562.8 bilioni.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Disemba 2023 uwiano wa deni la Taifa kwa thamani halisi kwa ukuaji wa uchumi umefikia kiwango cha asilimia 24 uwiano wa malipo ya deni ya Taifa kwa makusanyo ya ndani umefikia asilimia 6. Kwa takwimu hizi, inaonesha deni la Zanzibar ni himilivu katika kipindi cha muda wa kati na mrefu, hasa kwa kuzingatia kuwa uwiano unaokubalika kwa nchi zenye uchumi mdogo inatakiwa usizidi asilimia 70.

## 4. UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2023/2024 ni mpango wa tatu wa Utekelezaji

wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP, 2021-2026). Kwa kipindi cha mwaka 2023/2024 Mpango wa Maendeleo ulipanga kutekeleza jumla ya Programu 31 kati ya hizo tatu ni mpya na miradi ya maendeleo 58 kati ya hiyo 19 ni miradi mipya. Kiasi cha TZS 1,521.99 bilioni zimepangwa kutumika kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo TZS 1,514.79 bilioni zitatumika katika Serikali Kuu na TZS 7.2 bilioni kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hii ni ongezeko la TZS 162.60 bilioni sawa na asilimia 12.0 ikilinganishwa na Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2022/2023 ya TZS 1,352.19 bilioni.

**Mheshimiwa Spika,** Fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Programu na Miradi ya Kimkakati ni TZS 915.87 bilioni sawa na asilimia 60.46 na Miradi Mengineyo ni TZS 454.92 bilioni sawa na asilimia 30.03. Miradi mengineyo inajumuisha miradi inayoendelea na ile ambayo Serikali ina dhima kwa Washirika wa Maendeleo. Aidha, TZS 144.00 bilioni zimepangwa kutumika kwa ajili ya **Mfuko wa Kulipa Madeni ya Miradi** ya Maendeleo yaani ***Debt Service Fund.***

### 4.1. Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai – Disemba 2023, matumizi ya miradi ya maendeleo yamefikia TZS 843.47 bilioni sawa na asilimia 108.77 ya lengo la miezi sita la TZS 692.43 bilioni sawa na asilimia 50 ya lengo la mwaka la TZS 1,514.79 bilioni. Kati ya fedha hizo TZS 426.64 bilioni sawa na asilimia 45 kutoka Serikalini na TZS 416.52 bilioni sawa na asilimia 55 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Aidha, kati ya fedha za Serikali TZS 90.00 bilioni zimewekwa katika.

**Mfuko wa Kulipa Madeni ya Miradi ya Maendeleo.**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imepanga kutekeleza maeneo matano ya kimkakati kwa mujibu wa Mpango wa Kitaifa wa miaka mitano 2021-2026, Hata hivyo, utekelezaji unaoelezewa hapa umejikita katika maeneo manne ambayo yametekelezwa katika kipindi hichi yakiwemo ya kuweka Mazingira Wezeshi na Kuimarisha Miundombinu; Rasilimali Watu na Huduma za Kijamii; Utawala Bora na Uhimilivu na Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu. **Kiasi cha TZS 581.56** bilioni zimetumika ikiwa sawa na asilimia 63 ya lengo la **TZS 915.87 bilioni** kama ifuatavyo:

### 4.1.1. Mazingira Wezeshi na Kuimarisha Miundombinu

Katika kuimarisha miundombinu, Serikali katika eneo hili imepanga miradi sita ya kimkakati kama ifuatavyo:

**i. Programu ya Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba.**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2023/2024 programu ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba imehusisha hatua za awali za ujenzi wa maegesho, njia za kupitia ndege na jengo la abiria. Programu imekadiriwa kugharimu kiasi cha TZS 160.0 bilioni (TZS 10.0 bilioni kutoka Serikalini na TZS 150.0 bilioni kutoka kwa Wakopeshaji ambao ni UKEF/Citi Bank). Hadi kufikia Disemba, 2023, TZS 146 bilioni zimetolewa sawa na asilimia 91.25 ya lengo. Kati ya fedha hizo TZS 13 bilioni kutoka Serikalini zimetumika kuwalipa fidia wananchi 649 kati ya 719 na wananchi 70 waliobaki hatua za uhakiki

zinaendelea. Aidha, kiasi cha TZS 133 bilioni kutoka kwa Wakopeshaji zimelipwa ikiwa ni malipo ya awali (advance payment) ya Mkandarasi kwa kuanza ujenzi (mobilization works).

ii. **Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu**

**Mheshimiwa Spika, Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024** programu hii imepangiwa kutumia TZS 249.38 bilioni (TZS 75.39 bilioni kutoka Serikalini na TZS 174.0 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na Wakopeshaji). Programu hii imejumuisha ujenzi wa barabara za Tunguu-Makunduchi km 53; Chake Chake-Mkoani km 43.5 na Fumba - Kisauni km 12. **Hadi kufikia Disemba, 2023; TZS 230 bilioni sawa na asilimia 92.21 ya lengo la kipindi cha tathmini zimetolewa ikiwa ni malipo ya awali kwa Mkandarasi.** Kati ya fedha hizo TZS 48.82 bilioni kutoka Serikalini na TZS 181.14 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa ujenzi wa barabara ya Wete-Chake Chake yenye urefu wa km 22.1 unaendelea. Hadi kufikia Disemba 2023, TZS 94.67 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (BADEA) zimetolewa na kutumika kwakazi ya usafishaji wa barabara asilimia 100; Uwekaji wa tabaka la chini la mwanzo la kifusi (G7) asilimia 80; uwekaji wa tabaka la juu la mwanzo la kifusi (G15) asilimia 25; Uwekaji wa tabaka la pili la kifusi (G45) asilimia 32; na Ujenzi wa kalvati asilimia 2, Madaraja asilimia 30 na mabomba ya kupitishia miundombinu mbali mbali asilimia 80 kwa urefu wa km 10. Kwa ujumla kazi ipo asilimia 27 ya utekelezaji.

### iii. Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu imepangiwa kiasi cha TZS 44.0 billioni kutoka Serikalini. **Hadi kufikia Disemba 2023, jumla ya TZS 10.7 bilioni sawa na asilimia 24.2 zimepatikana. Kazi ya uwekaji wa lami km 10.0 imekamilika sawa na asilimia 100 ya shabaha kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2023.** Tathmini imefanyika kwa barabara nne ambazo ni Mwakaje –Mwachealale- Bumbwisudi, Kidoti, Mfurumatonga-Milele – Skuli –New Road na Dunga Zuze.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Pemba kazi za usafishaji wa kilomita 89.95 zinaendelea zikiwemo (Pembeni-Pandani(3.3km),Mzambarautakao-Mchangamdogo (6.0km), Mapofu-Tumbe-Kojifa-Bandarini (12.7km), Finya-Kicha (8.6km), Micheweni-Shumba Mjini-Bandarini (2.5km), Micheweni-Kiuyu – Maziwa Ng'ombe (7.5km), Konde-Msuka (4.1km).Kiungoni-Tovuni(1.5km), Penjewani-Mjini Kiuyu (2.2km), Mkarafuu Mmoja-(5.15km),Gando-Chokaani (2.1km), Gando-Chaoni, (1.5km); Bwagamoyo-Kele (6.5km), Ukutini-Mtangani-Bandarini(4.0km), Uondwe-Nyali (1.5km), Barawa-Mleteni (2.0km),Mgagadu-Kwautao (5.6km), Makongeni-Kinazini (3.2km) na Wesha-Mkumbuu (10km).

### iv. Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, programu imepangiwa kiasi cha TZS 80.1 bilioni kutoka Serikalini. Hadi kufikia Disemba 2023; kiasi cha TZS 56.58 bilioni zimeingizwa sawa na asilimia 70.64 ya makadirio. Kazi ya matengenezo ya barabara ya Kiembe Samaki njia panda kuelekea Amani - Mtoni na njia panda kuelekea barabara ya Mkapa km 8.5 pamoja na uwekaji wa lami km 5 kwa baadhi ya maeneo umekamilika na kufanya utekelezaji kufikia asilimia 30.14.

**Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa barabara ya Abeid Amani Karume Airport – Kiinua Miguu – Magereza unaendelea kwa ujenzi wa mitaro ya kupitishia maji kwenye kingo za barabara pamoja na njia za kupitishia miundombinu ya mawasiliano na maji. Utekelezaji wa km 6.5 za barabara hiyo umefikia asilimia 99.

**Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa Barabara ya Mazizini Vitambulisho – Zanzibar Beach Resort – Soko la Samaki umefikia asilimia 55, barabara ya Mwanakwerekwe GAPCO – Mwanakwerekwe Skuli–Kanisani kwa Mchina umefikia asilimia 78. Barabara ya Mombasa km 6.2 imefikia asilimia 40 ya utekelezaji. Matengenezo ya barabara ya Michenzani-Gongoni-Kisiwandui-Msikiti Mabati yanaendelea na yamefikia asilimia 60 hadi sasa. Kazi ya ujenzi wa barabara mbili za juu (fly over) km 10.78 katika mzunguko wa Mwanakwerekwe inaendelea kwa ujenzi wa nguzo na uchimbaji wa mashimo kwa ajili ya kuweka kitako cha kuweka nguzo na mzunguko wa Amani wanakamilisha utafiti.

**v. Ujenzi wa Bandari ya Mangapwani;**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2023/2024 kiasi cha TZS 20 bilioni zimepangwa kutoka Serikalini. **Hadi kufikia Disemba, 2023 TZS 13.36 bilioni** sawa na asilimia 66.8 zimelipwa kwa Mkandarasi. Kazi ya uhakiki wa tathmini ya fidia kwa Barabara ya Mashariki na Kusini inayohusisha nyumba na vipando maeneo ya Mangapwani, Kidanzini na Makoba inaendelea. Fedha za fidia zitalipwa baada ya kukamilika uhakiki. Kazi za upelekaji wa huduma za maji na umeme tayari zimeshafanyika katika eneo hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Disemba 2023, ujenzi wa barabara katika eneo la ndani ya bandari (ring road) km 12 zimejengwa sawa na asilimia 30. Kwa upande wa barabara ya magharibi katika eneo la bandari kazi zilizokamilika ni kuweka tabaka la msingi (sub base) kwa km 4.4 za barabara, ujenzi wa Culverts saba (7), ujenzi wa misingi ya kupitisha maji ya mvua (Concrete Channel) unaendelea kujengwa kwa kiasi cha mita 2,500. Kwa upande wa njia ya kaskazini mwa bandari yenye kilomita 1.2, kiasi cha mita 950 zinaendelea kujazwa kifusi kwa tabaka la chini (15 bottom - subgrade).

**vi. Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati ZESTA**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka **2023/2024, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 16.08 bilioni (TZS 7.20 bilioni kutoka Serikalini na TZS 8.88** bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (Benki ya Dunia). Kazi ya kuandaa michoro na kumtafuta mkandarasi wa ujenzi wa laini ya mkondo mkubwa wa umeme yenye uwezo

wa kilovolti 132 kutoka Welezo-Matemwe na Welezo-Makunduchi imefanyika na taratibu za zabuni zinaendelea kumpata mkandarasi wa uzalishaji wa umeme wa jua ambapo eneo tayari limeshapatikana lenye ukubwa wa hekta 18 Makunduchi. Ripoti ya awali ya tathmini imeshaandaliwa na kuwasilishwa Benki ya Dunia. Shehia zitakazoathirika ni 21 na waathirika 1,024.

**vii. Ujenzi wa Masoko na Vituo Vya Wajasiriamali**

**Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa masoko umejumuisha masoko matatu (Mwanakwerekwe B+G+2, Jumbi B+G+1 na Chuini B+G+1) ambayo yanakadiriwa kutumia  mpaka kukamilika kwake. Hadi kufikia Disemba 2023, **kiasi cha TZS 30.26 bilioni** zimetumika kwa ujenzi wa masoko hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa utekelezaji wa mradi, Soko la Mwanakwerekwe limefikia asilimia 67 ya ujenzi ambapo kwa sasa upo katika hatua ya uwekaji wa nondo katika ghorofa ya pili, uwekaji wa miundombinu ya paa na ujenzi wa maduka kwa eneo la ghorofa ya chini (ground floor) na ghorofa ya kwanza (first floor). Soko la Jumbi limefikia asilimia 70 ya ujenzi upo katika hatua ya uwekaji wa nondo katika ghorofa ya kwanza na Soko la Chuini limefikia asilimia 80 ambapo kazi ya upigaji wa plasta inaendelea. Ujenzi wa vituo vya wajasiriamali 14 vimejengwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kufikia Disemba 2023, vituo vyote vimekamilika na vimefunguliwa.

### 4.1.2. Rasilimali Watu na Huduma za Kijamii

**Mheshimiwa Spika,** Katika uimarishaji wa huduma za kijamii, Serikali imekusudia kuimarisha Sekta ya Elimu, Afya, Michezo, Miundombinu ya usambazaji

maji safi na salama pamoja na kutilia mkazo Mpango Shirikishi wa Kukuza Uchumi Zanzibar (BIG-Z).

Serikali katika eneo hili imepanga miradi sita ya kimkakati kama ifuatavyo:

### i. Programu ya Kuendeleza Viwanja vya Michezo

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2023/2024 programu imepangiwa kutumia **TZS 34.28 bilioni** ambapo **TZS 33.0 bilioni** kutoka Serikalini na TZS 1.28 bilioni kutoka kwa Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ). Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2023, programu hii imeingiziwa kiasi cha **TZS 27.87 bilioni** sawa asilimia 81.30. Kazi ya ukarabati wa Uwanja wa Amani pamoja na ujenzi wa viwanja viwili vipya kwa eneo la nje vimekamilika. Kazi zinazoendelea ni pamoja na ukamilishaji wa milango ya maduka; hoteli na mikahawa ili kukabidhiwa kwa Serikali kwa ajili ya matumizi rasmi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa sasa hatua za awali zinaendelea za ujenzi wa viwanja vya michezo vidogo vidogo (6-in-1 multi-sport centres) vya Wilaya za Unguja na Pemba vyenye hadhi ya kisasa. Viwanja hivyo vitajumuisha michezo ya basketball, handball, baseball, volleyball na netball.

Hadi kufikia Disemba 2023, kazi zilizofanyika ni upimaji wa viwanja, kuandaa michoro na kukamilisha BoQ. Aidha, kwa viwanja vya Matumbaku Sports Complex vimekamilika na tayari vimeshafunguliwa na kwa upande ukarabati wa Uwanja wa Gombani unaendelea na hatua ya utekelezaji.

**ii. Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi Katika Hospitali za Wilaya na Mkoa**

**Mheshimiwa Spika,** Programu ina lengo la kuimarisha makaazi kwa wafanyakazi ili kuongeza ufanisi na kupatikana muda wote itakapotokea dharura. Programu imeanza mwaka 2022/2023 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2023/2024. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, jumla ya **TZS 20.0 bilioni** zimetengwa kutoka Serikalini. Programu imejumuisha Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya Mkoa – Lumumba; hospitali ya Wilaya – Pangatupu; hospitali ya Wilaya - Mwera Pongwe; Hospitali ya Wilaya – Kitogani; Hospitali ya Wilaya – Vitongoji; na Hospitali ya Wilaya – Kinyasini.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai- Disemba 2023, hatua zilizofanyika ni kumpata Mkandarasi, Mshauri Elekezi pamoja na kusainiwa kwa Mikataba ya ujenzi. Mkandarasi amekabidhiwa maeneo ya ujenzi mwezi wa Disemba 2023. Kwa sasa Ujenzi wa nyumba za madaktari umeanza ukiwa katika hatua mbali mbali.

**iii. Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa – Binguni;**

**Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Binguni, hadi kufikia Disemba 2023, upembuzi yakinifu umekamilika na utiaji saini wa kupata mkopo umefanyika baina ya Serikali ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania na Jamhuri ya Watu wa Korea. Mradi unatarajiwa kutumia **USD 164 milioni** na ujenzi utakuwa ni wa miaka mitatu (2024-2027).

### iv. Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Elimu;

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuinua viwango vya elimu kwa kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunza. Kwa mwaka 2023/2024 Programu hii imepangiwa kutumia kiasi cha TZS 131.23 bilioni (TZS 59.04 bilioni kutoka Serikalini na TZS 72.19 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (AfDB, BADEA na World Bank)). Kwa kipindi cha Julai-Disemba 2023, jumla ya TZS 64.39 bilioni sawa asilimia 49.06 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa skuli 31 za ghorofa zikiwemo 12 za msingi na 19 za Sekondari. Kati ya fedha hizo TZS 50.72 ni kutoka Serikalini na TZS 10.72 bilioni zimetolewa na Washirika wa Maendeleo. Ujenzi unaendelea katika skuli 25 ambazo ziko katika hatua mbali mbali. Kwa ujumla ujenzi umefikia asilimia 60. Ujenzi wa nyumba 20 za walimu umefanyika kwa kujengwa nyumba 10 na ujenzi umefikia asilimia 50. Ujenzi wa madarasa 12 mapya ya Msingi katika maeneo ya Kisakasaka (8) na Umbuji (4) unaendelea na umefikia asilimia 80. Kwa upande wa Ujenzi wa Dakhalia katika Skuli za Paje - Mtule na Chwaka-Tumbe unaendelea katika hatua za ukamilishaji na umefikia asilimia 90 na ujenzi wa ofisi ya Wizara ya Elimu Pemba unaendelea na umefikia asilimia 40 na ujenzi wa ofisi ya Wizara ya Elimu Unguja hatua za kumtafuta mshauri elekezi zinaendelea.

### v. Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2023/2024, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 22.810 bilioni

kutoka Benki ya Dunia. Hadi kufikia Disemba 2023, kiasi TZS 13.4 bilioni zimepatikana sawa na asilimia 58.7 ya lengo, kazi ya ununuzi wa vifaa vya usafi (magari ya taka, makontena ya kuwekea taka na gari la kusafishia barabara) kwa Mabaraza ya Miji na Manispaa Unguja na Pemba imefanyika. Kampuni zilizoshinda zimeshajulishwa kwa ajili ya kusambaza vifaa hivyo. Jumla ya loti 3 kati ya 5 zitasambazwa vifaa hivyo, na loti mbili (2) zilizobaki zinategemewa kutangazwa tena kutokana na wazabuni kutofikia vigezo vilivyowekwa. Taratibu za kufanya manunuzi kwa loti mbili (2) tayari zimeshaanza. Vile vile, kazi ya kufanya upembuzi yakinifu wa uendelezaji wa urithi wa kihistoria ya Mji Mkongwe (Green Corridor) tayari Ofisi ya mradi imeshapata ithibati (approval) ya Mkataba kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi umekamilisha kazi ya kufanya mapitio ya usarifu wa michoro kwa Mradi wa Kuendeleza Maeneo yanayokuwa kwa kasi Zanzibar (Area Upgrading Unguja).Vile vile katika utekelezaji wa Mradi wa Ziwa Maboga na Mwantenga, mradi umekamilisha taratibu za kumpata Mshauri Elekezi. Rasimu ya mikataba imeshawasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kupata ithibati na kuendelea na hatua zinazofuata.Kazi hii inategemewa kutekelezwa kwa muda wa miezi saba (7).
Kutokana na athari za mvua kubwa zilizonyesha Zanzibar katika mwezi wa Novemba 2023. Benki ya Dunia imeridhia ombi la Serikali la kufanya uhaulishaji wa fedha kutoka Mradi wa BIG-Z katika kipengele cha Emergency and Contigency ili kukabiliana na athari za maafa zilizojitokeza kutokana na mvua kubwa. Serikali kwa kushirikiana na Benki

ya Dunia tayari imeshafanya tathmini (rapid assessment) ya athari za maafa yaliyojitokeza, mpango kazi wa utekelezaji wa mpango wa matumizi ya dharura tayari umeshaandaliwa. Aidha, Mradi umekamilisha kufanya tathmini (valuation) kwa waathirika wa maeneo ya Ziwa maboga na Mwantenga kwa ajili ya kuwalipa fidia na kuwahamisha katika eneo hilo. Hata hivyo, fidia za waathirika hao zinatarajiwa kulipwa kwenye utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Ziwa Maboga na Mwantenga.

**vi. Programu ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa jumla ya **TZS 29.66 bilioni** (TZS 11.16 bilioni kutoka Serikalini na TZS 18.50 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (Exim Bank-India).

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai-Disemba 2023, jumla ya TZS 22.05 bilioni zimeingizwa sawa na asilimia 74.3. Kati ya fedha hizo TZS 6.0 bilioni sawa asilimia 53.8 kutoka Serikalini na TZS 16.05 bilioni sawa asilimia 86.8 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kazi zilizofanyika na kukamilika ni uchimbaji wa visima 64 katika maeneo ya Dole (8), Kidutani (14), Dimani (5), Mfenesini (10), Maungani (9), Mkorogo (8) na Masingini (10); Ujenzi wa matangi 15 ya maji kwa LOT 1 (Mfenesini na Dole) umefikia wastani wa asilimia 95; kwa upande wa LOT 2 (Mkorogo, Maungani, na Dimani) umefikia wastani wa asilimia 97; na LOT 3 (Kidutani na Masingini) ujenzi wa matangi umefikia wastani wa asilimia 99. Kazi ya ulazaji wa mabomba imefikia wastani wa kilomita 450.81 kati ya kilomita 466.9 sawa na asilimia 96.5 ya

makadirio ambapo kwa LOT 1 (Mfenesini na Dole) zimefikia kilomita 176.57 na kwa LOT 2 (Mkorogo, Maungani, na Dimani) kilomita 151.34 na LOT 3 (Kidutani na Masingini) kilomita 122.9 na tayari baadhi ya wananchi wameshaunganishiwa maji kwa majaribio.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, ujenzi wa jengo la Ofisi za Makao Makuu ya Mamlaka ya Maji (Maji House) umekamilika kwa wastani wa asilimia 92. Kazi za kukamilisha jengo hilo zinaendelea kwa kumalizia kazi za ndani ya jengo (finishing).

**vii. Uimarishaji wa Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2023/2024, mradi huu umepangiwa TZS 10.50 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi sita (Julai-Disemba 2023) jumla ya TZS 1.78 bilioni sawa na asilimia 17 zimeingizwa kutoka Serikalini. Kazi zilizofanyika ni kuanza mradi kwa kazi ya usanifu wa mradi, kazi inayofanywa na Mshauri Elekezi.Makubaliano ya kuanza usanifu wa mradi yamefikiwa na usanifu wa mradi unaendelea na Mshauri Elekezi kutoka Kampuni ya Nippon Koei anaendelea na kazi hiyo. Mradi huu unafadhiliwa kwa fedha za mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (JICA).

**viii. Mradi wa Usalama wa Maji Zanzibar**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi unatekelezwa kwa pamoja baina ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) na Benki ya Maendeleo ya nchini Ujerumani (KfW) kwa gharama za Euro 660,000. Kazi ya upembuzi yakinifu wa usalama wa maji na kina cha maji chini ya ardhi

imekamilika. Hadi kufikia Disemba 2023, makubaliano ya kuanza mradi kwa kuweka miundombinu ya maji kwa Skimu 4 za Pemba yamefikiwa na utagharimu Euro 25 milioni (grant). Hatua za ukaguzi na tathmini ya maeneo ya mradi imeshafanyika.

### 4.1.3. Utawala bora na Uhimilivu

Katika kuimarisha Utawala bora na Uhimilivu, Serikali katika eneo hili imepanga kutekeleza miradi miwili kama ifuatavyo: -

**i. Mradi wa kuimarisha Ulinzi na Usalama**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa kiasi cha **TZS 20.0 bilioni** kutoka Serikalini kwa kutekeleza shughuli za kuweka miundombinu mipya ya mawasiliano ya ulinzi na usalama; ununuzi wa vitendea kazi vya operesheni vya Idara Maalum za SMZ; na kusimamia uendeshaji wa Mradi wa Mji Salama. Hadi kufikia Disemba 2023, jumla ya **TZS 8.33 bilioni** sawa asilimia 41.65 zimetumika. Mikataba ya ununuzi wa vifaa tayari umeshasainiwa na Kampuni ya Dash Communication Limited na Kampuni ya Burleth Limited.

**ii. Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2023/2024, programu imepangiwa jumla ya TZS 74.12 bilioni kutoka Serikalini. Serikali itajenga Mji wa Serikali katika eneo la Kisakasaka na jumla ya TZS 55.0 bilioni zimetengwa kwa ajili ya kugharamia ujenzi huo kwa kazi za matayarisho. Kiasi cha TZS 19.0 bilioni zimepangwa na kuanza kutumika kugharamia ujenzi wa majengo mbali mbali ya Serikali yakiwemo Ofisi ya

Mufti, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Ofisi ya Shirika la Nyumba.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miezi sita (Julai-Disemba) 2023, kiasi cha **TZS 2.67 bilioni** sawa na asilimia 41 zimepatikana kwa makadirio ya TZS 6.49 bilioni. Kazi zilizofanyika ni kuandaa michoro kwa ajili ya Skuli ya Sheria Zanzibar, kumlipa mkandarasi (KMKM) malipo ya awali kwa kujenga Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na ukamilishaji wa jengo la Ofisi ya Mufti unaendelea kwa kuweka miundombinu ya umeme, maji, kamera, plasta na matayarisho ya kuweka dari. Kwa upande wa Ujenzi wa Mji wa Serikali Michoro tayari imekamilika pamoja na kusafisha eneo kwa ajili ya kuanza ujenzi**.**

### 4.1.4. Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu

i. **Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Usarifu wa Dagaa pamoja na malipo ya boti**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha tathmini kiasi cha TZS 2.0 bilioni Fedha zimeingizwa kwa ajili ya utekelezaji wa Ujenzi wa Diko na Soko la kisasa, ambapo TZS 605 milioni zimetumika kwa kuwawezesha wajasiriamali kupitia Programu ya Uviko 19 kwa maeneo ya Uwekezaji na Uwezeshaji ikiwemo; Ujenzi wa Mabwawa ya Ufugaji wa Kaa na Matango bahari pamoja na kuwajengea Uwezo wafugaji na TZS 795 milioni zimetumika kwa ulipaji wa fidia kwa wananchi walioathiriwa na vipando vyao na mali katika maeneo ya Ndagoni Pemba, Kama, Fungurefu na Bwereu pamoja na kwa wananchiwa Charawe.

**Kiambatisho namba 2** kinaonesha utekelezaji wa miradi ya vipaumbele na miradi mengineyo.

## 5. UTEKELEZAJI WA BAJETI JULAI-DISEMBA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea na mkakati wa utafutaji na upatikanaji wa rasilimali fedha Ndani na Nje ya Nchi, kupitia dirisha la Mikopo nafuu kwa ajili ya kuhakikisha tulichoahidi ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020-2025 ***tunayatekeleza kwa ziada.*** Sambamba na kutekeleza mikakati mahsusi ya Maendeleo ya Zanzibar iliyoainishwa katika; Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, Mpango wa Maendeleo ya Zanzibar 2021-2026 (ZADEP), Mpango wa Mwaka wa Maendeleo 2023-2024 pamoja na maelekezo ya viongozi wakuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali ilikadiria kukusanya na kutumia TZS 2,840.85 bilioni Kati ya fedha hizo TZS 2,822.85 bilioni kutoka Serikali Kuu na TZS 18.00 bilioni kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

### 5.1. Mapato

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai-Disemba 2023, Serikali imefanikiwa kukusanya TZS 1,660.67 bilioni sawa na asilimia 58 ya bajeti ya kukusanya TZS 2,840.85 bilioni kwa mwaka, na asilimia 120 kwa makadirio ya Julai-Disemba 2023 ya kukusanya TZS 1,383.70 bilioni. Mapato yaliyokusanywa katika kipindi cha tathmini yameonesha ukuaji wa asilimia 141 ikilinganishwa na mapato ya TZS 683.36 bilioni yaliyokusanywa kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/2023.

### 5.1.1. Mapato ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2023/2024, Mamlaka ya Mapato Zanzibar imekadiriwa kukusanya TZS 675.60 bilioni. Hadi kufikia mwezi wa Disemba 2023, Mamlaka imekusanya TZS 351.77 bilioni sawa na asilimia 52 ya lengo la mwaka na asilimia 105 kwa makadirio ya Julai-Disemba 2023. Mapato yaliyokusanywa yameongezeka kwa TZS 65.63 bilioni sawa na ukuaji wa asilimia 23 ikilinganishwa na TZS 286.14 bilioni zilizokusanywa katika kipindi cha tathmini kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

### 5.1.2. Mapato ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Upande wa Zanzibar

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai-Disemba 2023, TRA kwa upande wa Zanzibar imekusanya TZS 250.85 bilioni sawa na asilimia 48 ya bajeti ya mwaka ya TZS 520.64 bilioni na asilimia 99 kwa makadirio ya kipindi cha tathmini ya TZS 253.39 bilioni. Mapato yaliyokusanywa yameonesha ukuaji wa asilimia 15.5 ikilinganishwa na TZS 217.24 bilioni zilizokusanywa kwa kipindi kama hichi kwa mwaka 2022/2023.

### 5.1.3. Mapato yasiyokuwa ya Kodi

**Mheshimiwa Spika,** Mapato yasiyokuwa ya kodi kwa kipindi cha miezi sita Julai hadi Disemba 2023, yamefikia TZS 81.53. bilioni sawa na asilimia 40 ya Bajeti ya mwaka ya TZS 201.79 bilioni na asilimia 86 kwa kipindi cha tathmini. Mapato hayo yanajumuisha Gawio la TZS150 milioni kutoka Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) Mapato hayo yanaonesha ukuaji wa asilimia 13 ukilinganisha na mapato ya TZS 72.05 bilioni zilizokusanywa kipindi kama hicho mwaka

2022/2023 ongezeko hili limetokana na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa kodi ya wafanyakazi wa SMT walioko Zanzibar makusanyo halisi ni TZS 8.75 makusanyo haya yamekuwa sawa na yaliyokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/2023.

### 5.1.4. Mapato kwa ajili ya Mfuko wa Miundombinu

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha mapitio ya bajeti hadi kumalizika mwezi wa Disemba 2023, Serikali imekusanya TZS 34.02 bilioni kutoka Mfuko wa Miundombinu sawa na asilimia 137 ya makadirio ya kukusanya TZS 24.87 bilioni kwa mwaka 2023/2024. Kati ya makusanyo hayo TZS 32.27 bilioni yamekusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) na TZS 1.75 bilioni kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa upande wa Zanzibar (TRA). Miongoni mwa Sababu ya kuongezeka kwa kodi hiyo ni kutokana na hatua zinazochukuliwa za kuongeza viwango vya utozaji kodi wa miundombinu kutoka USD 1 kwa kiwango cha awali na kufikia USD 2 hadi USD 5 kulingana na hadhi ya hoteli kwa Mgeni anayelala katika Hoteli za Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha miezi sita ukusanyaji wa Mapato umeonekana kuiamarika zaidi ukilinganisha na kipindi kilichopita, hii ni kwa sababu ya jitihada na mikakati inayoendelea kutumika kwa taasisi zinazosimamia ukusanyaji wa mapato. Miongoni mwa sababu hizo;

i. Kuimarika kwa shughuli za kiuchumi na uwekezaji wa miundombinu Zanzibar

unaotokana na utekelezaji wa sera nzuri za kiuchumi za Serikali ya Awamu ya Nane.

ii. Kuongezeka kwa Uwajibikaji wa walipakodi kwa kutimiza wajibu wao wa kulipa kodi kwa Hiari;
iii. Kuongezeka kwa ufanisi wa watumishi wa ZRA kutokana na utekelezaji wa Muundo mpya wa ZRA, Uboreshaji wa huduma za kodi katika ofisi za Mikoa ya kikodi ya Unguja na Pemba, pamoja na matumizi ya mifumo ya ukusanyaji kodi ya VFMS na ZIDRAS; na
iv. Kuimarika kwa ushirikiano na Taasisi nyingine zinazofanya kazi na ZRA ikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kamisheni ya Utalii na Ofisi za Uhamiaji.

### 5.1.5. Mkopo wa Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi kupitia Utaratibu wa Mkopo wa ndani

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali imepanga kukopa TZS 717.21 bilioni ikiwa ni mikopo kwa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo, kupitia mikopo ya Hati fungani na mikopo ya kibiashara. Hadi kukamilika kwa robo ya pili kiasi cha TZS 545.66 zimepatikana sawa na asilimia 126 ya kipindi cha Tathmini na asilimia 76 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo hati fungani tumepokea TZS 57.87 bilioni na Mikopo mengine kutoka NBC na NMB tumepokea TZS 487.79 bilioni.

### 5.1.6. Mapato ya Washirika wa Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilitarajia kupokea TZS 473.5 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha Julai-Disemba 2023 fedha zilizopokelewa ni TZS 416.52 bilioni sawa na asilimia

61 ya makadirio ya mwaka na asilimia 167 kwa kipindi cha tathmini. Mapato yaliyokusanywa yameongezeka kwa TZS 337.01 bilioni sawa na asilimia 451 ikilinganishwa na TZS 75.51 bilioni zilizokusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**Mikopo Nafuu ya Kisekta**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imepokea mikopo yenye thamani ya TZS 389.75 bilioni sawa na asilimia 74 ya bajeti ya mwaka na asilimia 222 kwa kipindi cha nusu mwaka. Mkopo huo uliopatikana unaonesha ukuaji wa asilimia 847 ukilinganishwa na mkopo wa TZS 41.12 bilioni uliopatikana kwa kipindi kama hichi kwa mwaka 2022/2023.

**Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imepokea TZS 26.77 bilioni sawa na asilimia 26 ya bajeti ya mwaka na asilimia 87 kwa kipindi cha nusu mwaka. Fedha hizi zilipokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali.

Kwa upande wa Misaada ya Kibajeti, Serikali haijapokea kiasi chochote kwa robo mbili za utekelezaji, hii inatokana na kutokamilika kwa taratibu kwa upande wa Tanzania bara. Matarajio ya mwanzoni mwa robo ya tatu fedha zitapatikana kwa ajili ya utekelezaji**. Kiambatanisho namba 3** kinaonyesha mchanganuo wa miradi iliyopatiwa fedha kutoka kwa Washirika wa maendeleo**.**

### 5.1.7. Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2023, makusanyo yamefikia TZS 5.58 bilioni

sawa asilimia 79 ya makadirio ya ukusanyaji wa TZS 7.10 bilioni ya makadirio ya kipindi cha tathmini.

### 5.2. Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** tumeshuhudia mageuzi makubwa ya kiuchumi na kijamii kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ikiwemo:-

i. Kuimarishwa kwa Huduma za Afya, Mageuzi ya sekta ya elimu, na upatikanaji wa maji safi na salama;
ii. Kuimarisha maeneo ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi;
iii. Kuboresha Miundo mbinu ya Barabara iliyounganisha na maeneo ya uzalishaji na Makaazi;
iv. Kudumisha hali ya Amani na utulivu katika Nchi yetu, na
v. Kuboresha vivutio katika maeneo ya wawekezaji katika sekta ya Utalii na Uchumi Buluu.

**Mheshimiwa Spika,** Dhamira Kuu ya Bajeti ya mwaka 2023/24 ni ***"Kujenga Uchumi Mpya Kwa Umoja, Mshikamano na Maridhiano"***. Katika utekelezaji wa dhima hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, chini ya Uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt.Hussein Ali Mwinyi imekuwa ikichukua jitihada mbali mbali katika kuhakikisha tafsiri na maana halisi ya Kauli "Yajayo Neema tupu" inaonekana katika Macho na Maisha ya Wazanzibari wote na wageni wanaoishi Zanzibar na pembezoni mwa Visiwa vya Unguja na Pemba.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai-Disemba Mwaka wa fedha 2023/2024, matumizi halisi yalifikia jumla ya TZS 1,437.36 bilioni, sawa na asilimia 51 ya

makadirio ya bajeti ya Mwaka ya TZS 2,840.85 bilioni na asilimia 108 ya kipindi cha tathmini. Matumizi haya yamejumuisha:-

### 5.2.1. Matumizi ya Kazi za Kawaida

Kwa upande wa matumizi ya kazi za kawaida TZS 588.78 bilioni zimetumika sawa na asilimia 45 ya bajeti ya 1,308.06 bilioni iliyopangwa kwa Mwaka na asilimia 94 kwa makadirio ya kipindi cha tathmini. Fedha hizo zimetumika kwa kazi za kawaida kwa ufafanuzi ufuatao:

**Mishahara kwa wafanyakazi wa Serikali;**

**Mheshimiwa Spika,** Mishahara ya Wafanyakazi katika kipindi cha Julai-Disemba 2023, makadirio yalikuwa ni TZS 286.51 bilioni hadi kufikia Disemba 30, kiasi cha TZS 286.38 bilioni kililipwa sawa na asilimia 99.9 ya makadirio.

**Mishahara kwa ajili ya Taasisi za Ruzuku;**

Taasisi za ruzuku katika kipindi cha Julai hadi Disemba 30, 2023 zilikadiriwa kulipa TZS 55.58 bilioni, malipo halisi ni TZS 55.13 bilioni sawa na asilimia 99 ya makadirio ya kipindi hicho.

**Matumizi ya Mafungu na Taasisi za Ruzuku;**

**Mheshimiwa Spika,** Jumla ya TZS 111.47 bilioni zilipangwa kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Mafungu hadi kufikia Disemba 31, 2023, TZS 82.55 bilioni zilitumika sawa na asilimia 74 ya makadirio, na Taasisi za Ruzuku zilikadiriwa kutumia TZS 46.69 bilioni na matumizi halisi yalifikia TZS 33.75 bilioni sawa na asilimia 72 ya makadirio ya kipindi hicho.

### 5.2.2. Matumizi ya Huduma Mfuko Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali umepangiwa kutumia jumla ya TZS 256.00 bilioni kwa mwaka wa fedha 2023/2024, kwa kipindi cha Julai-Disemba, 2023, TZS 130.97 bilioni zimetumika sawa na asilimia 102 ya kutumia TZS 128.22 bilioni katika kipindi hicho na asilimia 51 kwa bajeti ya mwaka. Fedha hizo zimetumika kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Malipo ya mafao ya Kiinua Mgongo TZS 15.41 bilioni kwa wastaafu 531 wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;

ii. Malipo ya Pencheni kwa wastaafu wa SMZ TZS 22.7 bilioni kwa wastani wa wastaafu 13,595 wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;

iii. Kulipa Pencheni Jamii TZS 9.09 kwa wastani wa wazee 29,312 wa Zanzibar;

iv. Matumizi mengineyo ya Serikali TZS 42.99 bilioni na

v. Kulipa riba ya hati fungani na mikopo ya Ndani TZS 40.78 bilioni.

#### 5.2.2.1. Malipo ya Deni na Dhamana za Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai-Disemba 2023 Malipo ya Deni la riba ya hati fungani na Mikopo ya ndani ni TZS 40.7 bilioni ikijumuisha:

i. Malipo ya marejesho ya mkopo wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii TZS 4.06 bilioni na

ii. Malipo na riba ya hati fungani na Mtaji TZS 32.66 bilioni,

iii. Malipo ya riba mkopo PBZ na NBC TZS 3.21 bilioni ,

iv. TZS 0.79 bilioni kwa malipo ya Wazabuni.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha**,** kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, Serikali imetoa dhamana ya TZS 78.01 bilioni kwa Taasisi zifuatazo:

i. Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) TZS 65.93 bilioni,

ii. Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA) **TZS 10.00 bilioni,**

iii. Kampuni ya Mwani (ZASCO) **TZS1.25 bilioni**

iv. Manispaa ya Magharibi “A’ **TZS 830 milioni**.

### 5.2.3. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha tathmini Serikali ilikadiria kutumia TZS 692.43 bilioni hadi kufikia Disemba 31, 2023 matumizi halisi yalifikia TZS 843.16 bilioni sawa na asilimia 122 ya makadirio ya TZS 692.43 kwa kipindi cha tathmini na asilimia 56 ya makadirio ya TZS 1,514.79 kwa mwaka. Fedha hizo zilitumika kugharamia utekelezaji wa Miradi mbalimbali, kati ya fedha hizo TZS 90 bilioni zimewekwa katika mfuko wa kuhudumia madeni.

**Mheshimiwa Spika,** Kati ya matumizi hayo, TZS 336.64 bilioni zinatokana na fedha za ndani sawa na asilimia 177 ya makadirio ya TZS 189.93 bilioni kwa kipindi hicho.

TZS 416.52 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ambapo Mikopo nafuu ya kisekta TZS 389.75 bilioni na TZS 26.77 bilioni ni Misaada.

### 5.2.4. Mfuko wa Kuhudumia Madeni (Debt Servicing Fund)

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imeanzisha mfuko maalumu kwa ajili ya kuhudumia mikopo ya ndani kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, katika hatua hio, Serikali ilipanga kuweka TZS 72 bilioni kwa ajili ya akiba kwa mwezi wa Julai hadi Disemba 2023, hadi kukamilika kwa robo ya pili jumla ya TZS 90 bilioni zimeingizwa katika hesabu maalum ya Mfuko wa Kuhudumia Madeni ili kulipia mikopo itakayochukuliwa na Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya maendeleo sawa na asilimia 125 ya makadirio. **Kiambatisho namba:5** Utekelezaji wa Bajeti Julai hadi Disemba 2023.

### 5.2.5. Mfuko wa Ustahamilivu wa Bei (Price Stabilization Fund)

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali imeanzisha Mfuko wa Uhimilivu wa Bei ili kuweza kusaidia kufidia gharama za ongezeko la bei linapotokea. Mfuko ulipanga kuchangiwa na mashirika mbali mbali kutokana na mapato yao, lakini hadi sasa, ni ZURA tu ndio walioweza kuchangia Mfuko huu. Hadi kufikia Disemba 31 una akiba ya TZS 3.2 bilioni ikiwa ni asilimia 15 ya mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA). Serikali kupitia Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango, inaendelea na kuandaa utaratibu mzuri zaidi wa taasisi zinazojitegemea na mashirika kuweza kuchangia Mfuko huu.

**Mheshimiwa Spika**, Muda mfupi ujao tutakabiliwa na mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhamani, kwa kawaida kipindi hicho tunakumbana na changamoto

kubwa ya kupanda kwa bei za vyakula hususan kwa bidhaa za mchele na sukari. Mfuko huu, utatumika kufidia gharama za bei za vyakula hivyo, kwa lengo la kupunguza makali ya mahitaji muhimu ya vyakula hivyo kwa msimu huu.

### 5.2.6. Mfuko wa Barabara

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Barabara nambari 2 ya mwaka 2001 yaliayofanywa kwa Sheria ya Mabadiliko Mbali Mbali ya Sheria Nam. 6 ya Mwaka 2023 majukumu ya iliyokuwa Bodi ya Mfuko huo yamekabidhiwa kwa Katibu Mkuu, Afisi ya Rais-Fedha na Mipango ambaye pia ndiyo Mlipaji Mkuu wa Serikali. Aidha, majukumu ya kupeleka fedha kwa Wakala wa Barabara kwa sasa yanasimamiwa na Katibu Mkuu na fedha zinazohitajika kwa ajili ya matengenezo ya barabara zinapelekwa moja kwa moja kwa Wakala wa Barabara kupitia kwa Katibu Mkuu hali ambayo imepelekea shughuli za matengenezo ya barabara kuendelea kama kawaida. Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2023 fedha zilizotumika kuupitia Mfuko huo ni TZS 5.89 bilioni.

### 5.2.7. Matumizi ya Mamlaka ya Serikali ya Mitaa

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika kipindi cha Julai-Disemba, 2023 TZS 5.41 bilioni zimetumika kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Mamlaka hizo. **Kiambatisho namba 4** Utekelezaji wa Mapato na Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Julai-Disemba 2023.

## 5.3. Mafanikio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali Kwa Kipindi Cha Julai - Disemba 2023

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai hadi Disemba utekelezaji wa Bajeti, Serikali imefanikiwa kutekeleza vipaumbele vya kimkakati sambamba na maeneo mengine ikiwemo:

i. Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati ikiwemo Miundo mbinu ya Barabara ambayo inarahisisha usafirishaji wa bidhaa na watu na kuunganisha Mikoa yote,
ii. Kufanikisha Mkutano wa Mapitio ya IDA 20 ambapo mikutano hiyo imeleta tija kwa Bajeti ya mwaka 2024/2025
iii. Kupatikana kwa huduma za kiuchumi na kijamii kwa programu na miradi iliyokamilika kwa muda uliopangwa;
iv. Kukua kwa uchumi na upatikanaji wa ajira mbali mbali,
v. Kupatikana kwa miundombinu bora katika utoaji wa Huduma za kijamii hususan katika sekta ya elimu na Afya,
vi. Ulipaji wa Mishahara na Madai ya Malimbikizo kwa watumishi wa Umma mapema na kwa wakati,
vii. Kupatikana kwa huduma ya maji safi na salama kwa maeneo mbali mbali ya visiwa vya Unguja na Pemba.
viii. Uwepo wa amani, umoja na utulivu ambao kwa kiasi kikubwa umepelekea utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Ufanisi na Haraka.

**Mheshimiwa Spika,** Mafanikio mengine yaliyopatikana Serikali kupitia mkakati wa kuwatumia wa Zanzibari wanaoishi nje ya Tanzania (Diaspora)

katika kuwawezesha kuisaidia Zanzibar kwa lengo la kuwekeza kwa ajili ya kuendeleza maendeleo ya nchi yao. Wanadiaspora wanaendelea kuitikia wito wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi unaowahimiza kurudi na kuchangia maendeleo katika nchi yao.

**Mheshiwa Spika,** Serikali imekuwa ikipokea michango tofauti kutoka kwa Wanadiaspora kwenye sekta za elimu, watu wenye mahitaji maalum, vyakula, na udhamini wa masomo kwa watoto yatima. Aidha, kupitia Sekta ya Afya, hivi karibuni tumeshughudia ujio wa Madaktari wataalamu wa ngozi, macho, kinywa na meno kutoka Marekani na kuwapatia matibabu wananchi zaidi ya 200, sambamba na kutupatia vifaa tiba, miwani na madawa vyenye thamani ya USD 200,000.

**Mheshimiwa Spika,** Wanadiaspora pia wamewekeza katika Sekta ya Elimu (Shule ya London Ladybird, Oplas Tanzania (mafunzo kwa kutumia TEHAMA)); Sekta ya Utalii (Ngalawa Hotel, JCB Hotel); Sekta ya Afya (Dr Mehta Hospital, Duka la Dawa RYTO); Sekta ya TeknoloJia (Rahisi Solution) pamoja na Kiwanda cha Chako, Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri wa Tanzania ziko katika uandaaji wa utaratibu maalum wa kuwapatia hadhi maalum wanadiaspora wa Tanzania wakiwemo wazanzibari, utakaowawezesha katika maeneo yafuatayo;

i. Kurithi, kurithiwa na kumiliki ardhi kwa njia ya lease,

ii. Kupata Kibali cha kuingia na kutoka Tanzania bila vikwazo,
iii. Kufungua account bank wakiwa ndani ya Tanzania,
iv. Kuasili (adoption), na
v. Haki ya kuwekeza kwa mtaji katika kiwango maalum.

## 5.4. Changamoto Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali Kwa Kipindi Cha Julai - Disemba 2023

**Mheshimiwa Spika,** Mbali na Mafanikio tuliyoyapata bado kuna changamoto kadhaa zikiwemo;

i. Kupanda kwa bei ya bidhaa mbalimbali zikiwemo bidhaa za chakula,
ii. Mwitikio mdogo wa wananchi wa kutoa na kudai risiti za kielektroniki kwa baadhi ya watendaji wa Serikali na Wananchi kwa ujumla,
iii. Mahitaji makubwa ya bajeti ya mishahara ikilinganishwa na bajeti halisi inayoidhinishwa hii inatokana na kubadilika miundo ya Taasisi na ongezeko kubwa la mishahara na maposho wakati wa Utekelezaji wa bajeti,
iv. Mafungu kuchelewa kufanya malipo kwa wazabuni na mahitaji mengine kutokana na changamoto za matumizi ya mifumo ya manunuzi,
v. Kuchelewa kuanza kwa baadhi ya miradi kutokana na kuchelewa kukamilika taratibu za awali ikiwemo mikataba, zabuni pamoja na kuondoshwa kwa miundombinu kwa ajili ya kupisha mradi,

vi. Kuchelewa kuanza kwa shughuli za uchumi wa buluu (uvuvi wa bahari kuu, michezo ya bahari na uchimbaji wa mafuta na gesi) na kumbi za mikutano,
vii. Kuchelewa kwa malipo ya fidia kwa wananchi waliopisha ujenzi wa miradi,
viii. Walimu kutoridhia kukaa katika nyumba za walimu kutokana na mazingira kuwa siyo rafiki,
ix. Ongezeko la gharama kwa baadhi ya miradi na kusababisha kutokukamilika kwa wakati na
x. Kukosekana kwa mpango wa uendelezaji wa mradi (Projects Sustainability Plan).

## 5.5. Hatua zilizochukuliwa kukabiliana na changamoto

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuchukua hatua kadhaa kukabiliana na kupunguza changamoto zinazojitokeza wakati wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali zikiwemo;

i. Kutoa elimu kwa wafanyabiashara na wananchi kuhusu umuhimu wa matumizi ya risiti za kielektroniki.
ii. Kuendelea kuboresha sheria za kodi, kuimarisha mifumo ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato.
iii. Kusimamia matumizi ya Serikali na kuondosha matumizi yasiyoleta tija.
iv. Kuendelea kushajiisha ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi mbali mbali.
v. Kuimarisha mifumo ya kidijitali katika kukusanya mapato, usimamizi wa bajeti pamoja na matumizi.

vi. Kusimamia ipasavyo, michakato ya manunuzi ili kuondosha uwezekano wa matumizi mabaya ya fedha kupitia ununuzi.
vii. Kupunguza ajira mpya kwa kada ambazo, watumishi wanapatikana katika sehemu nyengine.
viii. Kudhibti uanzishwaji wa taasisi mpya ambazo majukumu yake yanaweza kufanywa na taasisi zilizopo na hii inakwenda sambamba na kuunganishwa kwa taasisi mbazo majukumu yake yanaweza kufanywa kwa pamoja.

## 6. MISAMAHA YA KODI

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai-Disemba, 2023, maombi 162 ya misamaha ya kodi kutoka taasisi za umma, na ya watu binafsi yamewasilishwa. Kati ya maombi hayo, maombi 112 yamekubaliwa kutokana na kukidhi masharti ya sheria na maombi 17 yamekataliwa kutokana na kutokidhi masharti ya Sheria. Aidha, maombi ya misamaha 33 iliyobakia haikukidhi utaratibu wa maombi ya misamaha ikiwemo kutokamilika kwa baadhi ya taarifa za maombi pamoja na kutokamilika kwa taratibu za ufuatiliaji wa maombi hayo. Katika kipindi hicho, misamaha yote iliyotolewa ilikuwa na thamani ya TZS 54.74 bilioni. Kumekuwa na ongezeko la misamaha ya kodi ukilinganisha na misamaha ya TZS 46.11 bilioni iliyotolewa katika kipindi kama hichi kwa mwaka 2022/2023. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa miradi ya uwekezaji na ujenzi hapa Zanzibar na miradi inayo fadhiliwa na Washirika wa Maendeleo ambapo zaidi ya asilimia 90 ya misamaha yote imeelekezwa katika maeneo hayo.

## 7. UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA SERA ZA MAPATO KWA KIPINDI CHA JULAI DISEMBA 2023

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, Serikali imeendelea kuchukua hatua kadhaa ili kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato. Hatua hizo zilihusu marekebisho ya sheria pamoja na kuimarisha usimamizi na utawala wa kodi.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na utekelezaji wa sera hizo kwa kipindi cha miezi sita Julai-Disemba. Miongoni mwa maeneo ambao yamechangia ongezeko la mapato ni pamoja na;-

a) **Marekebisho ya Sheria ya Fedha Namba 9 ya Mwaka 2015**

i. **Kutoza Kodi ya Miundombinu kwa Uingizaji wa Bidhaa Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kuweka kiwango cha asilimia moja (1%) ya Kodi ya Miundombinu kwa Uingizaji wa Bidhaa Nchini. Hadi kufikia Disemba 2023, Serikali imefanikiwa kukusanya kiasi cha **TZS 1.754** bilioni kutokana na kodi hiyo.

ii. **Kurudisha Kiwango cha Awali cha TZS 100 ya Kodi ya Miundombinu kwa Lita ya Mafuta ya Dizeli na Petroli**.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho na utekelezaji wake umeanza Julai, 2023. Aidha, hadi kufikia Disemba, 2023 jumla ya **TZS 1.618** bilioni za ziada zimekusanywa kutokana na utekelezaji wa hatua hii.

iii. **Marekebisho ya Viwango Vya Kodi ya Miundombinu kwa Wageni Wanaolala Katika Hoteli za Zanzibar.**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kuweka viwango tofauti vya kodi kwa wageni. Hadi kufikia Disemba, 2023 kiasi cha TZS 16.219 bilioni za ziada zimekusanywa kutokana na utekelezaji wa hatua hii.

**b) Marekebisho katika Sheria ya Tozo la Petroli Nam. 7 ya Mwaka 2001**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kurudisha viwango vya awali vya Tozo la Petroli, Tozo la Kuendeleza Barabara na Ada ya Usajili wa Njia kwa uingizaji wa mafuta ya Dizeli na Petroli. Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2023; TZS 19.015 bilioni za ziada zimekusanywa kutokana na utekelezaji wa hatua hii.

**c) Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Stempu Nam. 7 ya Mwaka 2017**

i. **Kuongeza Kiwango cha Presumptive Tax Scheme kutoka Mauzo Ghafi ya TZS 5 Milioni hadi TZS 100 Milioni.**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kuongeza kiwango cha **Presumptive Tax Scheme** kutoka mauzo ghafi ya TZS 5 milioni hadi TZS 100 milioni. Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2023, walipakodi 7,820 wameingia kwenye utaratibu huu na kuchangia kodi yenye thamani ya TZS 0.276 bilioni **Kiambatisho namba 6** kinaonesha kwa kina utekelezaji halisi wa hatua za kuimarisha mapato kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2023.

## 8. MABADILIKO YA MAFUNGU YA BAJETI KWA KIPINDI CHA JULAI –DISEMBA MWAKA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa Vipaumbele kwa mwaka 2023/2024, kwa kipindi cha Julai-Disemba kumejitokeza upungufu wa makisio ya Bajeti iliyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa baadhi ya Miradi muhimu ya kimkakati. Hivyo, kupelekea kufanyika kwa mabadiliko ya mgawanyo huo wa rasilimali Fedha kwa baadhi ya Mafungu kwa kufanya uhaulishaji wa bajeti (virement) ili kukidhi mahitaji ya msingi ya miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Mabadiliko mengine yamejitokeza katika utekelezaji wa Bajeti ya Mishahara, Ikumbukwe kuwa mwaka 2023/2024 Serikali ilianzisha Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF), ambapo mtumishi katika Sekta ya Umma alitakiwa kuchangia asilimia 3.5 kutoka katika mshahara wake na asilimia 3.5 kutoka kwa muajiri yaani Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na kuchelewa kukamilika kwa hatua za kifedha za Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar Mchango wa Serikali wa asilimia 3.5 haukujumuishwa katika Bajeti za sekta husika, badala yake fungu hilo liliidhinishwa katika kifungu cha Marekebisho ya Mshahara. Hatua hii imepelekea mafungu yote ya Taasisi kubadilika bajeti iliyoidhinishwa hapo awali kwa kifungu cha mishahara. Hata hivyo, mabadiliko hayo yote hayakuathiri bajeti ya jumla ya Serikali ya mwaka 2023/2024. **Kiambatisho Namba 7** kinaonesha mabadiliko hayo kwa kila fungu.

## 9. MPANGO WA SERIKALI WA UNUNUZI WA MAGARI

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango imepewa jukumu la kufanya ununuzi wa gari zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilitengwa Bajeti ya TZS 22.041 bilioni kwa ajili ya ununuzi wa gari ambazo zitatumika kwa viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango katika kutekeleza jukumu hili, iliingia mkataba na Kampuni nne tofauti juu ya usambazaji wa gari kwa matumizi ya Viongozi pamoja na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kampuni hizo ni kutoka ndani na nje ya nchi ambapo kampuni tatu kutoka Tanzania ambazo ni Bucket Tanzania Limited, TATA Afrika Holidings Limited na FK Motor LTD na Kampuni ya SAS Afrika General Trading Limited kutoka nchini Dubai.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2023, Serikali imepokea jumla ya magari **65** kutoka kwa Kampuni zote 4 zilizoingia mkataba. Ambapo kampuni ya SAS Afrika General Trading Limited tumepokea gari 15 dhidi ya gari 31 zilizo hitajika gari hizo ni Land Cruizer Prado VXR tano na Land Cruizer Prado TXL (10) ambazo zote hizo zimeshawasilishwa Ofisi ya Rais-Ikulu na kubakisha gari kumi na sita (16) ambazo zinatarajiwa kuwasili muda wowote kuanzia sasa.

**Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Bucket Tanzania Limited, ilikuwa na mkataba wa gari 42 hadi Disemba 2023, Ofisi imepokea gari zote aina ya (Toyota Pick Up

Hilux 32 na Land Cruizer Mkonga 5 door 10) ambapo gari hizo zimeshakabidhiwa katika Wizara na Taasisi za Serikali ambazo ziliomba kupatiwa gari hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kutoka Kampuni ya TATA Africa Holdings (Tanzania) Ltd tumepokea gari 6 kwa matumizi ya Taasisi za Serikali gari hizo zote, zitakabidhiwa kwa Wizara na Taasisi ambazo zilihitaji kununuliwa gari hizo aina ya TATA BUS, ambapo kwasasa tunasubiri kupatiwa kibali kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kusafirishwa kutoka Bandari ya Dar es Salaam na kuwasili Bandari ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Kampuni ya Zenj Motors katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2023, hadi sasa kampuni imeshawasilisha gari 2 pekee kati ya gari 47. Aidha gari 45 zilizokuwa zinatarajiwa kupokewa zimeshindwa kuwasili kwa muda uliotarajiwa kutokana na changamoto mbali mbali zilizotokana na kampuni hiyo. ikiwemo; Uhaba wa Dola kwa ajili ya manunuzi, usafirishaji na vikwazo vya biashara kutoka wakala wa Kampuni ya Toyota Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na changamoto hizo, Serikali imechukua hatua ya kuvunja mkataba na Kampuni hiyo ya Zenj Motors kwa kuzingatia vipengele vya mkataba husika. Kwa sasa mkakati wa Serikali ni kuchukua mkopo nafuu kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar wa jumla ya USD 4.5 milioni kwa lengo la kufanya ununuzi wa gari 150 za aina ya 'KIA'. Gari hizo zinatarajiwa kufika mwishoni wa mwezi wa Machi, 2024.

## 10. MPANGO WA SERIKALI WA MATUMIZI YA ARDHI

**Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya ardhi ni moja la eneo ambalo linaleta changamoto kubwa hususan wakati wa utekelezaji wa Miradi ya kimakati ambapo matumizi mabaya ya Ardhi yanaigharimu Serikali hususan ulipaji wa fidia kwa wananchi, Serikali imeandaa mpango madhubuti wa kuhakikisha changamoto zilizopo Serikali, imejipangia kutekeleza bajeti kupitia Sekta ya Makaazi kwa kuandaa Mpango wa maalum wa kujenga nyumba Elfu Moja (1000) za bei nafuu na Biashara ambazo zitajengwa katika maeneo tofauti Unguja na Pemba. Nyumba hizo zitajengwa katika maeneo ya Kisakasaka ambapo zinatarajiwa kujengwa nyumba 172, Kiembe Samaki nyumba 40, Nyamazi 104, Mfikiwa 120, Kwahani 178, na Chuini 386.

**Mheshimiwa Spika,** Muelekeo wa Serikali ni kuimarisha na kusimamia matumizi bora ya Ardhi ili yawe katika mfumo wa usawa na endelevu kwa ajili ya kuleta maendeleo jumuishi, sambamba na kuyapanga na kuyapima maeneo kwa shughuli mbalimbali za Serikali, Kijamii na Kiuchumi kwa maendeleo endelevu ya matumizi ya Ardhi.

Miongoni mwa shughuli ambazo zimepangwa kutekelezwa ni pamoja:-

i. Kuandaa mpango maalum wa matumizi ya ardhi;
ii. Kutayarisha ramani na mabango na kusambaza katika maeneo yatakayopendekezwa kwa ajili ya maeneo ya ardhi ya akiba;
iii. Kuimarisha matumizi ya teknolojia ya kisasa katika kubuni na kutayarisha miundombinu na mifumo itayowezesha watumiaji kupata taarifa

za ardhi kwa wepesi.

## 11. MATARAJIO YA MAPATO NA MATUMIZI JULAI-JUNI KWA MWAKA 2023/2024

### 11.1. Mapato

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa mwenendo wa makusanyo, hadi kukamilika kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali inatarajia kukusanya TZS 2,838.53 bilioni katika kipindi cha Julai 2023 hadi Juni 2024 sawa na asilimia 99 ya makadirio.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuhakikisha Serikali inafikia malengo ya ukusanyaji yaliyowekwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024; taasisi zetu za ukusanyaji wa mapato zimepanga kutekeleza mikakati ifuatayo;

i. Kusimamia miongozo na maagizo ya viongozi wetu wa juu sambamba na kuimarisha mahusiano mazuri na walipakodi, matumizi ya Mifumo katika usimamizi wa kodi ikiwemo matumizi ya Risiti za Kielektroniki (VFD), matumizi ya mfumo wa ZIDRAS, na kukamilisha uunganishaji (integration) wa baadhi ya mifumo ya wafanyabiashara na Mfumo wa VFMS;

ii. Kuimarisha huduma za kodi (Elimu ya Kodi, Usajili wa Kodi, Uwasilishaji wa Ritani, Malipo ya Kodi na Ukaguzi wa Kodi) katika ofisi za kodi za Mikoa na vituo vya huduma za kodi (Tax Service Centres), pamoja na kuimarisha ZRA (call centres) ili kurahisisha ulipaji kodi wa hiari Zanzibar;

iii. Kuendeleza Weledi wa Watumishi wa ZRA kwa kuwapatia mafunzo stahiki, usimamizi makini, huduma nzuri kwa walipakodi (Customer care) pamoja na kuchukua hatua zinazofaa; na

iv. Kusimamia uwajibikaji wa hiari kwa walipakodi wakubwa, wakati na wadogo kwa kuwasaidia kurahisisha biashara zao na usimamizi wa usawa katika ulipaji kodi.

### 11.1.1. Mapato ya Ndani

Mapato ya ndani yanatarajiwa kufikia TZS 1,437.32 bilioni sawa na asilimia 101 ya makadirio ya bajeti.

**Mapato ya kodi**

**Mheshimiwa Spika,** Mapato ya kodi yanatarajiwa kufikia TZS 1,248.18 bilioni, sawa na asilimia 102.5 ya bajeti ya TZS 1,217.24 bilioni, kwa mchanganuo ufuatao:

i. Mamlaka ya Mapato Tanzania-Zanzibar (TRA) inatarajiwa kukusanya TZS 516.2 bilioni ikiwa asilimia 99.1 ya mapato hayo;

ii. Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) inatarajiwa kukusanya TZS 710.98 bilioni ikiwa ni asilimia 105.2; na

iii. Kodi ya Mapato kutoka kwa wafanyakazi wa SMT inatarajiwa kufikia TZS 21 bilioni sawa na asilimia 100 ya lengo.

**Mapato yasiyokuwa ya kodi**

**Mheshimiwa Spika,** Mapato yasiyokuwa ya kodi yanatarajiwa kufikia TZS 189.14 bilioni ikiwa ni asilimia 94 kwa mchanganuo ufuatao: -

i. Mapato ya Mawizara yanategemewa kufikia TZS 159.14 bilioni ikiwa ni asilimia 103.8 ya makadirio ya mwaka ya TZS 153.28 bilioni;

ii. Gawio la Mashirika ya Serikali linatarajiwa kufikia TZS 22.5 bilioni ikiwa ni asilimia 64.3 ya makadirio ya mwaka ya TZS 35 bilioni;

iii. Gawio la Benki Kuu ya Tanzania, linatarajiwa kufikia TZS 7.5 bilioni ikiwa ni asilimia 55.6 ya makadirio ya mwaka ya TZS 13.5 bilioni;

### 11.1.2. Mapato Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo yanatarajiwa kufikia TZS 678.71 bilioni sawa na asilimia 99 ya makadirio ya TZS 686.61bilioni, kwa mchanganuo ufuatao;

i. Misaada inatarajiwa kufikia TZS 79.17 bilioni, sawa na asilimia 75.4 ya Makadirio ya TZS 104.94 bilioni;

ii. Mfuko wa Pamoja wa Washirika wa Maendeleo (Basket Fund) unatarajiwa kufikia TZS 0.24 bilioni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya TZS 0.24 bilioni na

iii. Misaada ya Kibajeti (General Budget Support) inatarajiwa kufikia TZS 58 bilioni sawa na asilimia 111 ya makadirio na

iv. Mikopo nafuu ya kisekta inatarajiwa kufikia TZS 541.3 bilioni, sawa na asilimia 102 ya makadirio ya TZS 529.24 bilioni.

### 11.1.3. Mapato Mengineyo

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mapato Mengineyo matarajio ni kupokea TZS 710.00 bilioni

sawa na asilimia 99 ya makadirio ya TZS 717.21 bilioni, kati ya mapato hayo; TZS 150 bilioni tunatarajia kupata kutoka mkopo wa Hati Fungani sawa na asilimia 100 ya makadirio ya mwaka mzima na Mkopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo TZS 560.00 bilioni sawa na asilimia 99 ya makadirio ya mwaka.

### 11.1.4. Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa matarajio ni kukusanya TZS 12.5 bilioni sawa na asilimia 69 ya makadirio.

## 11.2. Matarajio ya Matumizi Januari - Juni 2024

**Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Serikali hadi kufikia Juni 2024 yanatarajiwa kufikia TZS 2,838.5 bilioni sawa na asilimia 99 ya bajeti ya mwaka ya TZS 2,840.85 bilioni.

Kati ya fedha hizo, TZS 1,314.37 bilioni zitatumika kwa matumizi ya kazi za kawaida sawa na asilimia 100 ya makadirio na TZS 1,511.66 bilioni zitatumika kwa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo sawa na asilimia 99 ya makadirio ya awali ( kati ya hizo TZS 692.49 bilioni ni kutokana na fedha za ndani, TZS 180 bilioni kwa ajili ya mfuko wa kugharamia madeni, ya miradi ya Maendeleo TZS 560 bilioni ni Mikopo na TZS 79.17 ni misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) na TZS 12.5 bilioni kwa matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Kwa uchambuzi wa matarajio ya mapato na matumizi hadi kufikia Juni 2024 **Kiambatisho namba 8** kinahusika.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Januri hadi Juni 2024, Serikali inatarajia kukopa TZS 164.34 bilioni kwa ajili ya kuziba nakisi ya bajeti, ambapo kati ya hizo Hati Fungani za Muda Mrefu ni TZS 92.13 bilioni na Mikopo ya Ndani ya kibiashara ni TZS 72.21 bilioni.

## 12. MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2024

### 12.1. Uchumi wa Dunia

**Mheshimiwa Spika,** Uchumi wa dunia unakadiriwa kubaki na kasi ya wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2024 kama ilivyokuwa mwaka 2023. Aidha, kwa mwaka 2024, kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi za Afrika Mashariki unatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 5.8 kutoka wastani wa asilimia 4.7 mwaka 2023

### 12.2. Mwelekeo wa hali ya uchumi wa Zanzibar 2024

**Mheshimiwa Spika,** Uchumi wa Zanzibar unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.2 mwaka 2024 kutokana na sababu zifuatazo:

i. Kuendelea kuwepo kwa hali ya amani na utulivu hapa Zanzibar, Tanzania, nchi jirani pamoja na utulivu duniani,

ii. Kuendelea kuongezeka kwa uingiaji wa watalii kwa asilimia 30 kutoka watalii 638,598 kufikia watalii 829,929,

iii. Kuongezeka kwa mapato ya ndani kutokana na kuongezeka kwa uwekezaji na utekelezaji wa mikakati ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali,

iv. Kuongezeka kwa uzalishaji viwandani na uchumi buluu,

v. Kuimarika kwa shughuli za kibiashara hasa kwa wajasiriamali wadogo wadogo kutokana na mikopo inayotolewa na Serikali, na

vi. Matumizi ya Serikali kuelekezwa katika shughuli za kukuza uchumi na huduma za kijamii.

### 12.3. Misingi ya Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2024/25

**Mheshimiwa Spika,** Misingi itakayozingatiwa kwa Mwaka 2023/24 ni kama ifuatavyo:

i. Ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara;

ii. Kuongezeka kwa uzalishaji wa ndani;

iii. Kuendelea kuimarika kwa usimamizi wa Sera za Kifedha;

iv. Kuimarika kwa upatikanaji wa nishati Zanzibar;

v. Kuendelea kuwepo kwa hali ya usalama katika nchi jirani;

vi. Kuendelea kuimarika kwa miundombinu ikiwemo bandari na kuimarika kwa uzalishaji katika sekta za uchumi buluu na

vii. Kuendelea kuwepo kwa amani na utulivu nchini.

## 12.4. Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi

**Mheshimiwa Spika,** Malengo na shabaha za uchumi jumla ni kama ifuatavyo:

i. Ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 7.2 mwaka 2024 kutoka makadirio ya ukuaji wa asilimia 7.1 mwaka 2023;

ii. Mfumuko wa bei kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja kama ilivyo shabaha iliyowekwa kwa nchi za Afrika Mashariki;

iii. Mapato ya ndani kufikia asilimia 18 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 kutoka matarajio ya asilimia 22.1 mwaka 2023/24;

iv. Mapato ya kodi kufikia asilimia 23 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 kutoka matarajio ya asilimia 22.4 mwaka 2023/24;

v. Uwiano wa Deni na Pato la Taifa kufikia asilimia 13 mwaka 2024/25 kutoka asilimia 15.2 mwaka 2023/24

vi. Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa chini ya asilimia 3.0 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25; na

vii. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje.

## 12.5. Mwelekeo wa Mfumko wa Bei Zanzibar

**Mheshimiwa Spika,** Kasi ya mfumko wa bei inatarajiwa kupunguwa na kufikia wastani wa asilimia 5.5 mwaka 2024 kutokana na sababu zifuatazo:

i. Serikali kuendelea kusimamia bei elekezi kwa bidhaa zinazoingia na kutumiwa nchini

zikiwemo bidhaa za chakula na baadhi ya vifaa vya ujenzi;

ii. Kuendelea kutekeleza Sera ya Fedha kupitia Benki Kuu ya Tanzania ili kudhibiti thamani ya Shilingi ya Tanzania;

iii. Kuimarisha programu za kilimo ili kuongeza uzalishaji wa ndani wa chakula;

iv. Kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Serikali kuendelea kudhibiti mwenendo wa sarafu ya Tanzania dhidi ya dola ya marekani; na

v. Kushajihisha uwekezaji wa viwanda kutokana na malighafi zinazopatikana ndani na nje ya nchi.

vi. Serikali Kusimamai Uingiaji wa chakula Nchini pamoja na kusimamia Bei zake kwa kutoa bei elekezi.

## 13. MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2024/2025 MAPENDEKEZO YA MAENEO YA KIMKAKATI

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2024/2025 Mpango wa Maendeleo utazingatia zaidi utekelezaji wa program na miradi ya maendeleo inayojikita zaidi katika kuimarisha hali za wananchi, kukuza ajira na kuongeza mapato ya Serikali ili kuwezesha kuleta matokeo ya haraka katika kuhakikisha maendeleo ya nchi na wananchi yanapatikana kwa haraka. Kwa mwaka 2024/2025, Mpango wa Maendeleo unategemea kutumia jumla ya TZS 2,455.68 bilioni sawa na asilimia 60.1 ya bajeti yote ya Serikali kwa mwaka 2024/25.

## 13.1. MAEENEO YA KIMKAKATI KWA MWAKA 2024/25

**Mheshimiwa Spika**, Mapendekezo ya maeneo ya kimkakati kwa Mpango wa Maendeleo ni kama ifuatavyo:

**i. Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu**

**a. Kuendeleza Utalii wa Baharini na Visiwani**

- Miradi ya Uwekezaji katika visiwa.
- Kuimarisha na kushajiisha ujenzi wa hoteli za nyota tano.
- Kuweka miundombinu ya kufanikisha michezo ya bahari.
- Kuanza maandilizi ya usafiri wa baharini (sea taxis).

**b. Kuimarisha Uvuvi na Rasilimali za Bahari;**

- Kuimarisha mazingira ya bahari.
- Kusimamia upatikanaji wa meli za uvuvi.
- Ununuzi wa boti mbili za abiria.
- Kujenga uwezo wa usimamizi wa rasilimali za bahari.
- Kuimarishwa kwa upatikanaji wa mazao ya baharini ikiwemo ukulima wa mwani, aquaculture na hatcheries.
- Kusimamia upatikanaji wa mifumo ya kuhifadhia mazao ya baharini.

**c. Kuendeleza Miundombinu ya Bandari;**

- Kuendeleza upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani.
- Utanuzi wa bandari ya Mkoani na Shumba
- Kusimamia na kuratibu ujenzi wa jengo la abiria la Mpigaduri.
- Kusimamia ujenzi wa bandari ya mizigo ya Fumba.

**d. Kuendeleza Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia.**

- Kuimarisha Shirika la Mafuta la Zanzibar (ZPDC).
- Kusimamia uwekezaji wa miundombinu ya uhifadhi wa mafuta na gesi asilia katika eneo la Mangapwani.

**ii. Mazingira Wezeshi na Uimarishaji wa Miundombinu**

**a. Kuimarisha Usafiri wa Anga;**

- Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Pemba, Nungwi na Jengo la Nne la Abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amaan Karume.
- Kusimamia ukamilishwaji wa ukarabati wa Jengo la Abiria la Pili.
- Kusimamia ukamilishwaji wa Jengo la Mizigo ya Ndege.

**b. Kuimarisha Usafiri wa Nchi Kavu;**

- Kuendelea na kusimamia ujenzi wa barabara kuu, mijini, vijijini na za ndani.
- Kuendelea na ujenzi wa vituo vya mabasi.

**c. Kuimarisha Miundombinu ya Maji na Umeme;**

- Ukamilishwaji wa miundombinu ya maji pamoja na usambazaji.
- Kuimarishwa kwa upatikanaji wa miundombinu na huduma za umeme.
- Upatikanaji wa umeme mbadala.

**d. Kuimarisha Miundombinu ya Utalii**.

- Kuimarishwa kwa maeneo ya kihistoria.
- Kuimarishwa miundombinu ya Mji Mkongwe.

- Kuanza ujenzi wa 'Zanzibar Convention Centre'.
- Ujenzi wa chuo cha Sanaa na utamaduni.

**iii. Kukuza Fursa za Kiuchumi**

**a. Ubunifu wa Uchumi wa Kidijital;**

- Kuendelea kuimarisha miundombinu ya uchumi wa kidijitali.
- Kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha na uendeshaji wa shughuli za Serikali.
- Ujenzi wa Vituo Vya Uhifadhi wa Taarifa.

**b. Kuendeleza Biashara na Viwanda.**

- Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya viwanda.
- Kuweka miundombinu kwa ajili ya Ujenzi wa maeneo ya viwanda.

**c. Kuimarisha uzalishaji katika kilimo**

- Kuendelea kukamilisha mageuzi ya kilimo hapa Zanzibar ili kukuza uzalishaji.
- Kushajiisha kilimo cha mazao mbadala ikiwemo kilimo cha viungo kwa ajili ya usafirishaji.
- Kuendelea kukamilisha miundombinu ya kilimo kwa ajili ya uzalishaji wa chakula kwa matumizi ya ndani.

**iv. Kuendeleza Rasilimali Watu na Huduma za Kijamii**

a. **Kuendeleza Miundombinu ya Afya**;

- Ujenzi wa nyumba za madaktari.
- Ujenzi wa Hospitali ya Binguni.
- Ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya.

**b. Kuendeleza Mageuzi ya Sekta ya Elimu;**

- Ujenzi wa Madarasa 1,000.

- Ujenzi wa dakhalia.
- Ukarabati wa skuli zilizochakaa.

**c. Ujenzi wa Nyumba zikiwemo za bei nafuu;**
- Ujenzi wa nyumba za bei nafuu katika maeneo ya Kwamchina, Kwahani, Mfikiwa na Chumbuni.
- Kushajiisha ushirikiano na sekta binafsi katika ujenzi wa nyumba za bei nafuu.

**d. Kuendeleza Sekta ya Habari na Michezo;**
- Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya,
- Kuanzisha vituo vya kulea na kukuza vipaji vya michezo,
- Ujenzi wa Jengo la ZBC na Tume ya Utangazaji.

**v. Kuimarisha Utawala Bora na Uhimilivu**

**a. Kuimarisha ulinzi na usalama**;
- Kuimarisha Ulinzi na Usalama.
- Ujenzi wa Mji wa Serikali na Ofisi za Wilaya.
- Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi za Serikali.

**b. Kuimarisha upatikanaji haki na usawa.**
- Ujenzi na Ukarabati wa Mahkama za Wilaya;
- Kuendelea na mifumo ya usimamizi wa kesi.
-

**c. Kuimarisha mazingira.**
- Mradi wa kuirithisha Zanzibar ya kijani.

## 14. MAPENDEKEZO YA SURA YA BAJETI MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya matumizi yanayowasilishwa katika Mwelekeo huu, kwa mwaka wa Fedha 2024/2025, yamezingatia uwezo wa mapato, kwa kuweka kipaumbele na mahitaji ya matumizi ya

lazima kwa mpangilio ufuatao; mishahara, mahitaji ya matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali na vipaumbele vya taifa. Vile vile mazingatio yapo katika maeneo mengine ikiwa pamoja na kugharamia Miradi ya Maendeleo inayoendelea na miradi yenye dhima na Washirika wa Maendeleo na miradi ya kimkakati inayoendelea na inayotarajiwa kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha pia mazingatio yamewekwa katika kugharamia utoaji wa huduma muhimu za kijamii ikiwemo afya, elimu, maji na kuimarisha maeneo muhimu ambayo yatapelekea kukua kwa uchumi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Mgao wa Bajeti katika mjumuisho wa Mapato na Matumizi umelenga kufanikisha shabaha na malengo ya Serikali katika maeneo yafuatayo :-

i. Maelekezo na Maagizo ya Serikali yanayotolewa na Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Kiujumla;
ii. Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020-2025;
iii. Utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa (ZADEP) 2021-2026.
iv. Vipaumbe vya taifa na vya kisekta,na
v. Mahitaji ya uendeshaji wa shughuli mtambuka.

### 13.1 Mwelekeo wa Ukusanyaji wa Mapato

**Mheshimiwa Spika,** Mapato ya Serikali kwa mwaka 2024/2025 yanakadiriwa kufikia TZS 4,085.80 bilioni ikiwa ni ongezeko la TZS 1,244.95 bilioni sawa na asilimia 43.8 ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka 2023/2024 ya TZS 2,840.85 bilioni. Kati ya fedha hizo,

TZS 1,700.79 bilioni zimekadiriwa kukusanywa kutoka katika vyanzo vya ndani, TZS 1,580.00 bilioni zinatokana na mkopo wa Ndani na Nje kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, TZS 805.01 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ikiwemo mikopo ya TZS 565.63 bilioni na misaada 151.11bilioni, TZS 0.27 bilioni zinatokana na Mfuko wa Pamoja wa Washirika wa Maendeleo na TZS 88 bilioni ni Misaada ya Kibajeti.

**Mheshimiwa Spika,** Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutokana na vyanzo vya tozo na ada yanakadiriwa kufikia TZS 22.179 bilioni.

### 13.2 Mapendekezo ya Mgao wa Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inatarajia kutumia jumla ya TZS 4,085.80 bilioni yakiwemo matumizi ya kawaida ya TZS 1,630.12 bilioni na matumizi ya maendeleo ya TZS 2,455.68 bilioni. Kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, matumizi ya kawaida ni TZS 13.41 bilioni na TZS 8.94 bilioni ni matumizi ya maendeleo. **Kiambatanisho Namba 9** kinaelezea Mapendekezo ya Sura ya Bajeti Kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024**.**

